

**MTAZAMO KUHUSU MATUMIZI YA KISWAHILI KUFUNDISHIA NA
KUJIFUNZIA MASOMO YA SEKONDARI: UCHUNGUZI KUTOKA
WILAYA YA KWIMBA MKOANI MWANZA**

JOSEPH PHILEMON

**TASNIFU IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MASHARTI
YA SHAHADA YA UZAMILI (MA.KISWAHILI) KITIVO CHA SANAA NA
SAYANSI YA JAMII, YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2023

UTHIBITISHO

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba amesoma Tasnifu hii yenye anuani **Mtazamo Kuhusu Matumzi ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Masomo ya Sekondari: Uchunguzi kutoka Wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza** na anapendekeza ipokelewe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya M.A (Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania



Dkt. Salma O. Hamad

(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa, hairusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa baadhi ya maandishi ya Tasnifu hii bila idhini ya Mwandishi wa Tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi **JOSEPH PHILEMON** natamka na kuthibitisha kwa Seneti ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwamba Tasnifu hii inayoitwa: **Mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Masomo ya Sekondari: Uchunguzi kutoka Wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza**, ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa pahala pengine kwa lengo la kutunukiwa shahada ya aina hii au nyingine yoyote.



Saini

Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii namtabaruki mama yangu mzazi **ANNA BISEKO MAZIGE** aliyenilea na kunifanya niwe na kiu ya masomo na maadili mazuri ya utumishi wa umma. Namtabaruku mke wangu **AMINA JUMA ALLY**. Nawataburuku pia wanangu **GOODLUCK JOSEPH** na **ROBINA JOSEPH** kwa uvumilivu na mchango wao katika kipindi chote cha masomo.

SHUKURANI

Kazi ya kukamilisha utafiti huu haikuwa kazi nyepesi bali kwa kushirikiana na watu mbalimbali kwa mawazo imeweza kukamilika. Kwanza, namshukuru Mungu kwa kuniwezesha afya njema kwa kipindi chote na hadi nakamilisha kazi hii. Pili, natoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Salma O. Hamad wa Chuo Kikuu cha Tanzania kwa kutumia uzoefu wake, Taaluma yake, muda na ushauri wake umewezesha kukamilika kwa Utafiti huu. Tatu, natoa shukrani kwa wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambao ni Dkt. Mohamed Maguo, Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Dunlop Ochieng na Dkt. Nasra Habibu waliotoa mihadhara na Maelekezo mbalimbali katika kipindi cha Masomo. Nne natoa shukrani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kwimba Bi. Happyness Msanga kwa kukubali kunipa kibali cha kufanya utafiti katika shule za sekondari zilizoteuliwa na utafiti huu. Nawashukuru wakuu wa shule, walimu, wazazi na wanafunzi wa shule za sekondari Malya, Mwandu, Maligisu na Tallo kwa ushirikiano waliouonyesha katika mchakato wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Mwisho, nawashukuru wanafunzi wenzagu wa Shahada ya uzamili ya Kiswahili 2019/2020 kwa ushirikiano wao katika masuala ya kitaaluma kwa kipindi chote cha masomo.

IKISIRI

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza Mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Walengwa wa utafiti huu walikuwa walimu, wanafunzi na wazazi katika shule za sekondari za serikali wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo ni; Kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari, kubainisha vikwazo vinavyokwamisha lugha ya Kiswahili isitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari na kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya hatua iliyofikiriwa ambayo imeaksi vyema kusudio la utafiti huu. Njia ya dodoso, mahojiano na uchunzaji darasani zilitumika kukusanya data. Uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo ulitumia mikabala ya kitakwimu na kimaelezo. Matokeo ya utafiti huu yalibaini sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari ni; Kiswahili kuwa lugha bora, Kiswahili kutawala mazungumzo, Kiswahili kuwa lugha mama, Kiswahili kuwa na msamiati toshelevu, Kiswahili ni lugha muhimu na Kiswahili kueleweka kwa urahisi. Pili, utafiti ulibaini vikwazo vinavyokwamisha lugha ya Kiswahili isitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari ni kulegalega kwa sheria ya lugha nchini Tanzania, udhaifu wa asasi na vyombo kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili, Kiswahili kutokuwa na hadhi, kulegalega kwa sera ya lugha na msukumo mdogo wa viongozi wa kisiasa. Tatu, utafiti ulibaini upo mtazamo chanya wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO LA MTAHINIWA.....	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xii
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Tatizo la Utafiti	5
1.4 Lengo Kuu la Utafiti	6
1.5 Malengo mahususi ya Utafiti	6
1.6 Maswali ya Utafiti.....	6
1.7 Umuhimu wa Utafiti	7
1.8 Upeo wa Utafiti.....	7
1.9 Muhtasari	8

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA

NADHARIA..... 9

2.1 Utangulizi.....	9
---------------------	---

2.2	Kazi Tangulizi Kuhusu Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia.....	9
2.3	Mtazamo kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia	11
2.4	Kiunzi cha Nadharia.....	13
2.4.1	Nadharia ya hatua iliyofikiriwa.....	13
2.5	Muhtasari	15
SURA YA TATU: MBINU NA NJIA ZA UTAFITI		16
3.1	Utangulizi.....	16
3.2	Aina ya Utafiti.....	16
3.3	Eneo la Utafiti	16
3.4	Sampuli na Usampulishaji	17
3.4.1	Sampuli	17
3.4.2	Mbinu za Usampulishaji	18
3.5	Njia za Ukusanyaji wa Data.....	20
3.5.1	Hojaji au Dodoso	20
3.5.2	Mahojiano	21
3.5.3	Uchunzaji Darasani.....	21
3.6	Vifaa vya Kukusanyia Data	22
3.7	Uchambuzi wa Data.....	23
3.8	Muhtasari	24
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA		25
4.1	Utangulizi.....	25
4.2	Kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	26

4.2.1	Data za sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili zilizokusanywa uwandani kwa njia ya dodoso la walimu	26
4.2.2	Data kuhusu sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia zilizokusanywa uwandani kwa njia ya dodoso la wanafunzi...	28
4.3	Kubainisha vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	31
4.3.1	Data za Vikwazo Vinavyokabili Kiswahili Zilizokusanywa Uwandani kwa Njia ya Dodoso la Walimu	31
4.3.2	Data za Vikwazo Vinavyokabili Kiswahili Zilizokusanywa Uwandani kwa Njia ya Dodoso ya Wanafunzi.....	35
4.4	Kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	38
4.4.1	Data ya mtazamo wa walimu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	39
4.4.2	Data ya mtazamo wa wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	42
4.4.3	Data ya mtazamo wa wazazi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	44
4.5	Data Zilizokusanywa kwa njia ya Uchunzaji Darasani	46
4.6	Muhtasari	47
SURA YA TANO: MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO		48
5.1	Utangulizi.....	48
5.2	Matokeo ya Utafiti	48

5.3	Mapendekezo	49
5.4	Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo	49
5.5	Hitimisho.....	50
MAREJEO.....		52
KIAMBATANISHO I.....		60
KIAMBATANISHO II.....		62

ORODHA YA MA JEDWALI

Jedwali Na. 3.1:	Mchanganuo wa Watafitiwa	20
Jedwali Na. 4.1	Kuonesha Majibu ya Walimu Kuhusu Sababu zinazoshawishi Matumizi ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Masomo ya Sekondari.....	26
Jedwali Na. 4.2	Kuonesha Majibu ya Wanafunzi Kuhusu Sababu zinazoshawishi Matumizi ya Kiswahili Kufundishia Na Kujifunzia Masomo ya Sekondari	28
Jedwali Na. 4.3	Kuonesha Majibu ya Walimu Kuhusu Dodoso la vikwazo vinavyoikabili Lugha ya Kiswahili Isitumike katika Kufundisha na Kujifunzia Masomo ya Sekondari	31
Jedwali Na. 4.4	Kuonesha Majibu ya Wanafunzi Kuhusu Dodoso la vikwazo vinavyoikabili Lugha ya Kiswahili Isitumike katika Kufundisha na Kujifunzia Masomo ya Sekondari.....	35
Jedwali Na. 4.5	Kuonesha majibu ya walimu ya mahojiano yaliyofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	39
Jedwali Na. 4.6	Kuonesha majibu ya wanafunzi ya mahojiano yaliyofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	42
Jedwali Na. 4.7	Kuonesha majibu ya wazazi ya mahojiano yaliyofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.....	44

ORODHA YA VIFUPISHO

BAKITA	Baraza la Kiswahil Tanzania
BODA	British Overseas Development Administration
LOITASA	Language of instruction in Tanzania and South Africa
Na.	Namba
NECTA	The National Examinations Council of Tanzania
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
TPH	Shirika la Uchapishaji Vitabu Tanzania
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii imejadili, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti uliofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundisha na kujifunza masomo ya sekondari.

1.2 Usuli wa Mada

Suala la ufundishaji lugha lilianza kutiliwa mkazo katika nchi za Kimagharibi mapema katika karne ya 14 wakati Kilatini ilipokuwa lugha peke ya matumizi katika shughuli za kibiashara, elimu, dini na utawala. Hata hivyo, katika karne ya 16 lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kiitaliano zilianza kutambuliwa kwa sababu ya mabadiliko ya kisiasa (Richard na Rodger 1986). Tafiti zilizofanywa na Gorman (1974) na Onyango (1990) nchini Kenya zilionyesha wazi kuwa wasomi wengi walikuwa na mtazamo hasi juu ya matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji na shughuli nyingine za kila siku. Hili lilichagizwa na kasumba ya waafrika kutukuza lugha za kimagharibi kuona ni lugha bora na zinafaa kutumika katika nyanja zote.

Naye Akaka (2017) anasema kuwa nafasi ya Kiswahili katika mfumo wa elimu kabla na baada ya uhuru nchini Kenya ilikuwa ikitegemea tume, hasa baada ya kuundwa kwa tume zilizotoa mapendekezo kuhusu mwelekeo wa elimu nchini. Kati ya tume nyingi zilizoundwa, zikiwemo ya Ominde (1964), Wamalwa (1972), Gachathi (1976) na Kamunge (1988). Tume ya Mackay (1989) na tume ya Koech (1999) zitabaki katika kumbukumbu za kihistoria kama tume zilizoendeleza sana Kiswahili nchini Kenya kwa kupendekeza Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za msingi na

sekondari. Nao Omulando (2002) na Simala (2006) tafiti zao zilionesha mwamko wa watu wakenya wa kuwa na mtazamo chanya juu ya matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na shughuli nyingine za kila siku.

Sewangi (2004) anaeleza kuwa, nchini Tanzania mwaka 1967 utakumbukwa katika historia kwa kutangazwa kwa Azimio la Arusha lililofafanua siasa ya ujamaa na kujitegemea. Ili kufanikisha elimu ya kujitegemea, suala la lugha lilihitaji kushughulikiwa na kuwekwa wazi. Katika kipindi hicho Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) lilianzishwa. Hadi kufikia mwaka 1968 kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya kufundishia elimu ya msingi. Kabla ya hapo Kiswahili kilitumika katika madarasa manne tu ya mwanzo katika shule za msingi huku kiingereza kikitumika katika madarasa yote ya juu. Msanjila (1990) anaongeza kuwa uamuzi mwingine ulifanyika baadae wa kuifanya lugha ya kiswahili itumike katika kufundishia vyo vya ualimu wa shule za msingi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu (1984) ilielekeza Kiswahili kitumike katika nyaja za kijamii na kisiasa, elimu ya msingi, vyo vya ualimu wa shule ya msingi na elimu ya watu wazima. Lugha ya Kiingereza ilipangiwa kutumika maeneo ya sekondari, elimu ya juu mahakama zote isipokuwa ya mwanzo, sayansi na teknolojia na diplomasia ya kimataifa. Utenganishaji huu ulipingwa vikali na baadhi ya wataalamu kama vile Mulokozi (1989) kuwa ulilenga kuitukuza lugha ya Kiingereza na kushusha hadhi ya lugha ya Kiswahili.

Kamwaga (2023) anafafanua kuwa nchini Tanzania, katika shule zote za umma mfumo ni wa kufundisha masomo yote kwa lugha ya Kiswahili katika ngazi ya shule

za msingi. Huku Kiingereza kikifundishwa kama somo. Kuanzia ngazi ya sekondari na kuendelea, lugha ya kufundishia huwa ni Kiingereza. Matarajio ya mfumo huu yalikuwa kwamba miaka saba ya kufundishwa somo la Kiingereza katika ngazi ya msingi ni maandalizi ya mwanafunzi aweze kufundishwa na kuelewa masomo mengine katika lugha ya Kiingereza atakapofika sekondari na vyuo. Kamwaga anaendelea kufafanua kuwa matarajio hayo ya kuelewa Kiingereza katika miaka ya awali hayafikiwi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita takwimu za Baraza la Mitihani ya Taifa la Tanzania (NECTA) zinaonesha idadi kubwa ya wanafunzi wanaomaliza mitihani ya shule ya msingi huwa hawafaulu somo la Kiingereza. Kamwaga anaendelea kusisitiza kuwa hata katika matokeo ya mtihani wa ngazi ya diploma ya ualimu nchini Tanzania, mara nyingi ufaulu huwa ni wa kuanzia kiwango cha daraja C kushuka chini. Utafiti wa Kawanga ulijikita zaidi kuchunguza Kiingereza kama somo na haukujikita kuchunguza Kiingereza kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Saleh (2019) anaeleza kuwa katika kufundishia lugha yoyote ile ya kigeni kunakuwa na changamoto mbalimbali wakati wa ufundishaji wake. Changamoto hizo huweza kusababishwa na mambo mengi ambayo yamo au yanajitokeza katika mchakato huo.

Kwa takribani miongo mitano tangu uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar kumekuwepo na mijadala na matamko mbalimbali kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia hapa nchini Tanzania. Mijadala hiyo inahusisha lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza ambazo kwa mujibu wa mpango lugha na sera ya lugha ya nchi zimetajwa kuwa lugha za kufundishia na kujifunzia kwa ngazi tofauti za elimu. Pamoja na kuwepo kwa mpango-lugha na sera ya lugha kueleza hivyo

uwepo na mijadala na matamko ya kila mara vinaashiria wazi kuwa lipo tatizo la lugha ya kufundishia na kujifunzia katika muktadha wa Tanzania hususani katika shule za sekondari. Tafiti zinaonesha kuwa matumizi ya lugha ya kiingereza yamekuwa na changamoto nyingi si kwa wanafunzi tu bali ni changamoto hata kwa walimu. Wataalamu mbalimbali wameshauri sifa na mahitaji muhimu ya lugha inayofaa kufundishia na kujifunzia. Senkoro (2004) anaeleza kuwa lugha ya kufundishia ni ile inayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi. Nao Brock-utne na wenzake (2003) wanaeleza kuwa lugha ya kufundishia ni suala la kipekee katika umuhimu wake wa kuwezesha wanafunzi kuuliza maswali, kujadili na kubainisha mada wao kwa wao au kushirikiana. Naye Mekacha (2000) anasisitiza kuwa, nyenzo pekee inayomwezesha binadamu kufikiri, kuwasiliana, kuhifadhi na kurithisha maarifa ni lugha. Tikolo (2012) anadai kwamba, ufahamu wa mwanafunzi wa lugha aliyoizoea wakati wa kukua kwake inaweza kuwa ni msingi wa ujifunzaji mzuri wa baadaye pale anapounganisha na ujuzi wa mwalimu wake. Nao Msanjila na wenzake (2011) wanadai kwamba, lugha ya kufundishia na kujifunzia inapoteuliwa visivyo, huwa kunajitokeza vikwazo vingi ambavyo hukwamisha ufanisi katika kutoa, kubuni na kuendeleza maaarifa. Kwa mujibu wa wataalam hao ni wazi kuwa kwa muktadha wa Tanzania uteuzi wa lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari haukuzingatia maoni hayo. Tafiti nyingi zimefanyika na kubainisha kuwa lugha ya Kiingereza ambayo iliteuliwa haikidhi haja ya walimu na wanafunzi kuitumia kama lugha ya mafunzo hii ni kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Qorro (2003), Malekela (2004) na Mwinshehe (2003) zinaeleza kuwa, matumizi ya lugha ya kigeni katika kufundishia yana changamoto katika ujenzi wa jamii imara katika maendeleo. Qorro anendelea kufafanua kuwa ipo mifano ya nchi ulimwenguni zilizoamua

kutumia lugha zake katika mfumo wa elimu na zimeonyesha mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii akitolea mfano nchi ya China. Kutokana na hoja hizo kutoka katika tafiti za wataalamu suala la lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari bado ni tatizo na hivyo linahitaji tafiti zaidi. Pamoja na kuwepo kwa tafiti zilizopendekeza matumizi ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari utekelezaji wake umesuasua pengine kutokana na baadhi ya wadau muhimu kutoshirikishwa kutoa maoni na mtazamo wao kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari hapa nhini Tanzania. Msukumo huu uliibua hisia kwa mtafiti kufanya utafiti ili kuchunguza mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

1.3 Tatizo la Utafiti

Tafiti zilizofanyika tokea miaka ya 1970 hadi 2000 kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia nchini Tanzania, na kwa uelewa wa mtafiti wa utafiti huu, hazikuchunguza mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari nchini Tanzania. Kukosekana kwa utafiti unaochunguza mtazamo ni kikwazo katika kutatua changamoto zinazotokana na lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Hivyo basi, utafiti huu ulinuia kuchunguza mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari kwa kuangazia mambo yafuatayo; kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari, kubainisha vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari na kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kuchunguza mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

1.5 Malengo mahususi ya Utafiti

Utafiti ulikuwa na malengo mahususi matatu ambayo mtafiti alishughulika nayo. Malengo hayo ni haya yafuatayo;

- i) Kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.
- ii) Kuchunguza vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.
- iii) Kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

1.6 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na swali ambalo ni je, kuna mtazamo gani kuhusu kufundishia na kujifunzia kwa Kiswahili masomo ya sekondari? Ili kufikia haja hiyo mtafiti aliongozwa na maswali mahususi matatu.

- i) Ni sababu zipi zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari?
- ii) Ni vikwazo gani vinavyokwamisha Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya Sekondari?
- iii) Jamii ina mtazamo gani kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza mtazamo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa wanafunzi, walimu, jamii, wanaisimu na serikali kama ifuatavyo;

Utafiti huu umetoa mwelekeo juu ya kukabiliana na tatizo la lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari kwa kubainisha sababu zinazoshawishi Kitumike badala ya Kiingereza kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Utafiti huu umeeleza wazi vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kisitumike. Hivyo vikwazo hivi vikiondolewa lugha ya Kiswahili itaweza kutumika.

Utafiti huu umebainisha wazi maoni ya wanajamii ya kuwa na mtazamo chanya wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Utafiti huu utawawezesha watunga sera kuchukua hatua za makusudi kurekebisha kasoro zilizopo katika uteuzi wa lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

1.8 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza mtazamo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Kijiografia utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Mwanza wilaya ya Kwimba katika kata ya Malya, kata ya Mwandu, kata ya Maligisu na kata ya Nyambiti. Sababu ya kuchagua kata hizi ni wakazi wengi wa kata hizi hutumia Kiswahili kama lugha yao ya pili na baadhi yao hutumia Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Shule zilizohusika katika utafiti huu ni shule

ya sekondari Malya iliyopo kata ya Malya, shule ya sekondari Mwandu iliyopo kata ya Mwandu, shule ya sekondari ya Maligisu iliyopo kata ya Maligisu na shule ya sekondari Tallo iliyopo kata ya Nyambiti.

Mipaka kitaaluma, mitazamo iliyochunguzwa ilihusiana na changamoto ya matumizi ya Kiingereza kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari, vikwazo vinavyosababisha Kiswahili kisitumike na kutathmini sababu za Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Wanafunzi waliotafitiwa ni wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne tu. Mtafiti aliwachagua wanafunzi wa kidato cha tatu na nne kwa sababu wanafunzi wa vidato hivi tayari wameshajifunza masuala ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Vile vile wamejifunza kwa lugha ya Kiingereza kwa muda mrefu kuliko wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili, hivyo wamekumbana na changamoto nyingi za kujifunza kwa lugha ya Kiingereza. Pia utafiti huu umehusisha walimu wa shule za sekondari wanaofundisha somo la Kiswahili, Historia, Jiografia pamoja na Baolojia. Walimu wa masomo haya walichaguliwa kwa sababu wao ndiyo wamilisi wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Pia, utafiti ulihusisha wazazi wa wanafunzi hao. Wazazi walichaguliwa kwa sababu wao wanakuwa na wanafunzi baada ya muda wa masomo.

1.9 Muhtasari

Katika sura hii ya kwanza, mtafiti ameweka bayana usuli wa mada juu ya lugha ya kufundishia na kujifunzia. Vilevile amejadili tamko la tatizo la utafiti wake kwa kuonesha pengo la utafiti. Malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti yamewekwa bayana. Mtafiti ameeleza kwa kina umuhimu wa utafiti wake pamoja na upeo wa utafiti wake.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii ina sehemu kuu nne, Sehemu ya kwanza mapitio ya kazi tangulizi kuhusu mtazmano wa lugha ya kufundishia na kujifunzia. Sehemu ya pili ni yaliyoandikwa kuhusu changamoto zinazokumba walimu na wanfunzi kuhusu matumizi ya kiingereza kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Sehemu ya tatu ni kiunzi cha nadharia iliyoongoza utafiti huu na sehemu ya nne ni muhtasari wa yaliyojadiliwa katika sura hii.

2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia

Msanjila na wenzake (2009) wanasema kuwa lugha ya kufundishia ni lugha inayotumika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu wa nchi. Lugha ya kufundishia ni msaada kwa wanaojifunza kuendeleza vipaji vyao, kukuza ubunifu na kukabiliana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Naye Qorro (2005) anaeleza kuwa lugha ya kufundishia ni chombo cha kupitishia elimu kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi na miongoni mwa wanafunzi wenyewe.

Senkoro (2004) anasisitiza kuwa lugha inayoweza ujifunzaji na ufundishaji ni ile ambayo inaeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi. Naye Mekacha (2000) anasisitiza kuwa, nyenzo pekee inayomwezesha binadamu kufikiri, kuwasiliana, kuhifadhi na kurithisha maarifa ni lugha. Tikolo (2012) anadai kwamba, ufahamu wa mwanafunzi wa lugha aliyozoea wakati wa kukua kwake inaweza kuwa ni msingi wa ujifunzaji mzuri wa baadaye pale anapounganisha na ujuzi wa mwalimu wake. Nao Msanjila na wenzake (2011) wanadai kwamba, lugha ya kufundishia na

kujifunzia inapoteuliwa visivyo, huwa kunajitokeza vikwazo vingi ambavyo hukwamisha ufanisi katika kutoa, kubuni na kuendeleza maaarifa. Kwa muktadha wa nchi ya Tanzania uteuzi wa lugha ya kufundishia masomo ya sekondari haukuzingatia maoni hayo. Tafiti nyingi zimefanyika na kubainisha kuwa lugha ya Kiingereza ambayo iliteuliwa haikidhi haja ya walimu na wanafunzi kuitumia kama lugha ya mafunzo.

Mlama na Matteru (1978) walichunguza haja ya kutumia Kiswahili kufundishia elimu ya juu. Katika utafiti huu walibaini hali ya matumizi ya lugha katika kufundishia na jinsi lugha ya kufundishia inavyoathiri elimu nchini Tanzania. Walitembelea shule, vyuo na ofisi za elimu katika mikoa kadhaa na kuzungumza na wanafunzi, walimu na viongozi wa elimu mikoani na wilayani. Walitoa pia hojaji ambazo zilijazwa na walimu na wanafunzi. Vile vile, walihudhuria vipindi madarasani. Katika utafiti huu, ilidhihirika bayana kwamba, stadi za lugha ya Kiingereza zimepungua kiasi kwamba mtindo wa kutuma lugha hiyo unatatiza wanafunzi pamoja na walimu. Matokeo ya hali hiyo ni kwamba hakuna ufanisi katika kufundisha na kujifunza. Hivyo, Wataalamu hawa walitoa mapendekezo mawili: Kwanza, Kiswahili kitumiwe kufundishia katika elimu ya juu, ili kutatua matatizo yanayosababishwa na matumizi ya lugha ya Kiingereza. Na vile vile, kuikuza na kuimarisha lugha ya Kiswahili kuifanya iwe lugha ya kitaalamu. Pia, kuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza, kwa vile tunahitaji lugha za kigeni katika mawasiliano ya kimataifa na katika kutupatia ujuzi zaidi.

Criper na Dodd (1984) walifanya utafiti kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia elimu ya sekondari. Uchunguzi wao ulijikita katika ujuzi wa lugha ya Kiingereza

walionao walimu na wanafunzi. Matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa walimu na wanafunzi hawana ujuzi wa kutosha wa lugha ya Kiingereza na kuhitimisha kuwa uamuzi wa kutumia lugha ya kiingereza haukuwa sahihi kama njia ya kutolea elimu katika ngazi hiyo. Naye Rubagumya (1991) alichunguza utumiaji wa lugha mbili yaani kiswahili na kiingereza katika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Katika utafiti wake aligundua kwamba walimu na wanafunzi wanalazimika kutumia lugha zote mbili ili kuwezesha maelewanao. Matumizi ya lugha ya kiingereza pekee hayakuwa na ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Rubagumya (2003) anasema baadhi ya walimu wa sekondari hawana uwezo wa kufundisha kwa lugha ya Kiingereza kwa ufasaha na hulazimika kutumia lugha mbili ili waweze kufafanua mada darasani. Tafiti zinabainisha kuwa walimu na wanafunzi wanakumbwa na changamoto za kutomudu stadi za kiingereza, kuwa na umilisi mdogo wa lugha ya kiingereza, kuchanganya na kubadili misimbo ya kiingereza na Kiswahili, lugha ya kiingereza kutoeleweka vizuri kwao na hata kwa jamii inayowazunguka. Hali hii inasababisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji kutofikiwa. Hivyo basi, tafiti hizi zilimsaidia mtafiti kuchunguza mtazamo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari ili kubaini mwikio wao.

2.3 Mtazamo kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia

Kwa mujibu wa utafiti huu neno mtazamo limechukuliwa kama mwelekeo, hisia au msimamo kuhusu jambo fulani. Hivyo basi, mtazamo kuhusu lugha ya kufundishia na kujifunzia ni mwelekeo, hisia au msimamo wa watu kuhusu lugha inayotumika au kupendekezwa kufundishia na kujifunzia. Gorman (1974) katika utafiti alioufanya

(1969) alichunguza suala la lugha katika elimu nchini Kenya, huku akitathmini matatizo mbalimbali katika ufundishaji wa lugha. Katika utafiti wake aligundua kuwa wanafunzi wengi walikuwa na mtazamo hasi na kwa vyovyote hawakutaka kujifunza lugha ya Kiswahili. Aidha, alitambua kuwa wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini Kenya walikuwa na ufahamu tofauti wa lugha ya Kiswahili, huku waliotoka mikoa ya Pwani, Bonde la Ufa, na Mashariki na shule za mabaraza ya Miji walikuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili wakilinganishwa na wa sehemu nyingine.

Onyango (1990) alichunguza mtazamo wa wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali, huku akiwashirikisha wahadhiri na maprofesa kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi kama wasailiwa. Katika utafiti huu, aligundua kuwa wasomi wengi walikuwa na mtazamo wa kutosisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kila siku. Utafiti wake ulibainisha kuwa wasomi kamwe hawakujitambulisha kwa lugha ya Kiswahili. Ildhihirika kuwa wasomi hawakuwa na mapenzi na lugha ya Kiswahili, bali lugha ya Kiingereza na mara nyingi walijinasibisha nayo. Aligundua kuwa walitumia lugha ya Kiingereza katika shughuli zao rasmi za kila siku. Hivyo, alihitimisha kwamba mielekeo yao ilikuwa hasi kuhusu lugha ya Kiswahili.

Watafiti hawa wanapingana na matokeo ya utafiti uliofanya na Omulando (2002) ambaye alichunguza athari za lugha ya Kiswahili katika Kiingereza katika kufundisha masomo ya sekondari wilaya ya Bungoma nchini Kenya. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa lugha ya Kiswahili imeanza kuchukua nafasi kama lugha ya kufundishia katika shule za mashambani (vijijini) na pia ni lugha ambayo

imepanuka kimatumizi. Simala (2006) alieleza kuwa lugha ya Kiswahili ina utajiri wa msamiati wa kufundishia na haina tatizo kama wengi wanavyoamini kuwa imepungukiwa msamiati faafu kwa masomo ya sayansi. Hivyo basi, Utafiti wa Omulando (2000) na wa Simala (2006) umebadili mtazamo na hisia hasi na kuibua mtazamo chanya wa matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Matokeo ya tafiti hizi yamechochea haja ya kuchunguza mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari kutokana na mapendekezo na matamko mbalimbali ya kubadili lugha ya kufundishia kutoka Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili kwa lengo la kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji. Hata hivyo, kwa uelewa wa mtafiti hakuna utafiti uliochunguza mtazamo walionao walimu, wanafunzi na wazazi juu ya mapendekezo ya kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari hapa nchini Tanzania.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Massamba (2009) anasema kuwa nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa mawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo fulani. Kwa kuwa nadharia ni dira na mwongozo, utafiti huu umeongozwa na nadharia ya hatua iliyofikiriwa (Theory of Reasoned Action) ya Ajzen na Fishbein (1975).

2.4.1 Nadharia ya hatua iliyofikiriwa

Nadharia ya hatua iliyofikiriwa imeasisiwa na Ajzen and Fishbein (1975) na kuendelezwa hadi (1980) wakieleza kuwa mtazamo wa binadamu katika jamii hutegemea imani aliyonayo kutokana na hali mbalimbali. Wanataja vyanzo vinavyoweza kubadili mtazamo wa binadamu kuwa ni uzoefu binafsi, elimu,

ushawishi kutoka katika vyombo vya habari na mwingiliano na jamii. Waliongeza kuwa imani inayojengwa na mtazamo fulani humfanya mtu kuamua kufanya au kutokufanya jambo alitakalo. Nadharia ya hatua iliyofikiriwa inaeleza kuwa binadamu ni kiumbe mwenye utambuzi na anaweza kutumia maarifa yake kwa utaratibu. Nadharia ya hatua iliyofikiriwa inaamini kuwa binadamu akifanya jambo ambalo litamnufaisha atakuwa na mtazamo chanya na akifanya jambo ambalo halimnufaishi atakuwa na mtazamo hasi. Nadharia hii ina mihimili mikuu mitatu ifuatayo;

- i) Ajzen na Fishbein (1980) wanaeleza kuwa kila mtu ana imani inayofungamanishwa katika matendo na tabia ambayo husababisha matokeo fulani. Hivyo mtu akiwa na imani kuwa jambo analolifanya lina manufaa atakuwa na mtazamo chanya na kama halina manufaa kwake atakuwa na mtazamo hasi.
- ii) Ajzen na Fishbein (wameshatajwa) wanadai kuwa mtazamo wa mtu ni matokeo ya tathmini chanya au hasi anayoifanya kwa kuangalia thamani halisi ya jambo fulani
- iii) Ajzen na Fishbein (wameshatajwa) wanaongeza kuwa dhamira ya mtu huweza kutathminiwa kwa kutumia vipengele viwili. Vipengele hivyo ni dhamira yake binafsi na ushawishi kutoka nje. Hii ina maana kwamba binadamu atakubaliana na jambo fulani kama jambo hilo linaungwa mkono na jamii na atakuwa na mtazamo hasi kama haliungwi mkono na jamii.

Katika utafiti huu, mtafiti ameitumia nadharia ya hatua iliyofikiriwa kwa sababu suala la uchaguzi wa lugha ya kufundishia na kujifunzia unahusisha imani, nia na

mtazamo alionao binadamu kuhusu matumizi ya lugha fulani na hivyo manufaa anayoyatarajia yanaweza kuathiri mtazamo aliyonayo. Hivyo basi, uchambuzi wa data za utafiti huu iliongozwa na nadharia hii katika malengo mahsusi na katika uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu. Malengo hayo ni:-

- i) Kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.
- ii) Kubainisha vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kisitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.
- iii) Kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

2.5 Muhtasari

Sura hii ya pili imejadili kwa kina mapitio ya kazi tangulizi. Katika mapitio ya kazi tangulizi, changamoto zinazowakumba walimu na wanafunzi wanapofundisha na kujifunza kwa lugha ya Kiingereza zimejadiliwa. Mtafiti amefafanua mtazamo juu ya lugha ya kufundishia na kujifunzia na kuweka wazi pengo lililozibwa na utafiti huu. Vile vile mtafiti ameifafanua nadharia ya hatua iliyofikiriwa na kuonesha namna ilivyotumiwa na mtafiti.

SURA YA TATU

MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii ina vipengele vikuu nane. Vipengele hivyo ni aina ya utafiti ambao mtafiti ameufanya, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, njia za kukusanyia data, vifaa vya kukusanyia data na uchambuzi wa data na hitimisho la sura hii.

3.2 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ni utafiti wa uwandani. Katika aina hii ya utafiti mtafiti alikutana na wasailiwa kwa kufanya nao mahojiano ya ana kwa ana pamoja na kuwapatia hojaji kwa lengo la kukusanya data ili kuweza kuchunguza mtazamo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sekondari. Katika utafiti huu wa uwandani mtafiti alikutana na wanafunzi wa elimu ya sekondari, walimu wao pamoja na baadhi ya wazazi wa wanafunzi hao.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika mkoani Mwanza katika wilaya ya Kwimba. Wilaya ya Kwimba ina jumla ya kata 30 na shule za sekondari za umma 34, katika wilaya hii ni kata nne tu kati ya kata thelathini zitazohusika katika utafiti huu. Kata zilizohusika pamoja na shule zake ni Kata ya Malya (shule ya sekondari Malya), Kata ya Mwandu (shule ya sekondari Mwandu), Kata ya Maligisu (shule ya sekondari Maligisu) na kata ya Nyambiti (shule ya sekondari Tallo). Kata hizi zilichaguliwa na mtafiti ili kuwa eneo lake la utafiti kwa sababu wakazi wake wengi hutumia lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili na baadhi lugha yao ni lugha yao ya kwanza katika mawasiliano

yao kwa muda mwingi. Hivyo, huenda ikawa na athari katika mtazamo wa matumizi kwenye nyanja ya ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sekondari.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Katika kipengele hiki idadi ya watafitiwa au wasailiwa imewekwa bayana, vilevile mbinu zilizotumika kuwapata wasailiwa au watafitiwa nazo ziliwekwa wazi na mtafiti.

3.4.1 Sampuli

William (2011) anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti (vinavyotafitiwa) yaani watu, taasisi, vitu au matukio. Kwa ujumla, kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Kothari (2004:55), anaelezea kuwa, uteuzi wa walengwa ni mbinu au utaratibu ambao mtafiti atatumia katika kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli. Kundi lengwa la utafiti huu lilijumuisha walimu wa sekondari 81, wanafunzi kidato cha tatu na cha nne 798 na wazazi wa wanafunzi 70 ambamo sampuli ya uwakilishi ilichambuliwa kwa kuzingatia maoni ya Sedlack na Stanley (1992) waliosisitiza kuwa katika uchaguzi wa sampuli ni sharti watafitiwa waeleweke kimalengo na kimazingira. Katika utafiti huu walimu walikuwa nguzo muhimu kwa vile wao ndio walio na mitagusano ya karibu na wanafunzi. Pia huwa na athari hasi au chanya, kupitia mtazamo wao kuhusiana na lugha ya Kiswahili na namna wanavyoitumia. Wazazi walikuwa miongoni mwa watafitiwa kwa vile huathiri matumizi ya lugha katika mazingira ya nyumbani. Wanafunzi walimpatia mtafiti picha halisi nyanjani iliyomwezesha kufahamu matumizi ya Kiswahili katika shule za wilaya ya Kwimba. Kwa hivyo habari zilizotolewa nyanjani zilimsaidia

mtafiti kutambua mtazamo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

3.4.2 Mbinu za Usampulishaji

Mtafiti aliteua sampuli ya utafiti kulingana na sifa za watafitiwa kuwa na uwezo wa kutoa data sahihi zilizotakiwa kulingana na lengo la utafiti yaani waliokuwa na uwezo wa kutoa habari faafu zilizojibu kikamilifu maswali ya utafiti. Babbie (1999) anasema kwamba, sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa.

Katika utafiti huu watafitiwa 108 waliteuliwa kwa mchanganuo ufuatao wanafunzi 80 waliteuliwa ikiwa ni asilimia 10 ya jumla ya wanafunzi 798 wa kidato cha tatu na cha nne kwa shule zilizoteuliwa. Walimu 16 ikiwa ni asilimia 19 ya jumla ya walimu 81 na wazazi 12 ikiwa ni asilimia 17 ya wazazi 70 waliteuliwa kutokana uwezo wa kutoa taarifa faafu katika kuwakilisha wengine na kuwezesha uthibiti data kutoka kwa watafitiwa kama wataalamu wanavyoshauri. Watafitiwa hawa walipatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa (wa makusudio), usampulishaji nasibu na usampulishaji kutajana. Miongoni mwao, watafitiwa 80 ambao ni wanafunzi wa shule za sekondari waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa (wa kimakusudi) na usampulishaji nasibu. Usampulishaji lengwa ulilenga wanafunzi wa kidato cha tatu na cha nne ambapo kila shule ilitoa wanafunzi 20 ambao waliteuliwa kwa sababu wao wamekuwa shuleni kwa muda mrefu wakijifunza kwa lugha ya kiingereza katika masomo yao na wamejifunza maendeleo ya lugha ya

Kiswahili. Hivyo basi, wanafahamu changamoto na fursa zilizopo katika lugha ya Kiswahili na kiingereza katika ujifunzaji wao. Katika usampulishaji nasibu mtafiti aliandaa vikaratasi vidogo vidogo vilivyoandikwa “ndiyo” na “hapana” na kuvichanganya changanya na kisha kuvitupa chini na kuwataka wanafunzi waokote vikaratasihivyo. Waliookota vikaratasi vilivyoandikwa neno “ndiyo” hao ndiyo waliohusika kama watafitiwa wa utafiti huu. Watafitiwa 16 walikuwa walimu wa shule za sekondari ambapo kila shule ya sekondari ilitoa walimu 4 ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa na usampulishaji kutajana. Walimu hao ni wale ambao wanafundisha masomo ya Historia, Baolojia, Jiografia na Kiswahili katika shule zilizoteuliwa. Sababu ya kuwateua walimu hawa ni umahiri walionao katika kufundisha na uzoefu wao katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Watafitiwa 12 walikuwa wazazi wa wanafunzi ambapo kila shule waliteuliwa wazazi 3. Hawa waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa na usampulishaji kutajana. Wanafunzi na walimu walisaidia kuwabaini wazazi hao na kuwapa mwaliko wa kuhudhuria shuleni. Wazazi waliteuliwa kwa sababu ni miongoni mwa wafuatiliaji wa karibu juu ya maendeleo ya taaluma kwa watoto wao. Hivyo wanaweza kueleza mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Watafitiwa

Na.	Kundi la watafitiwa	Idadi ya watafitiwa	Waliojaza dodoso	Walishiriki mahojiano ya ana kwa ana
1.	Wanafunzi wa shule za sekondari	80	80	40
2.	Walimu wanaowafundisha wanafunzi	16	16	16
3.	Wazazi wa wanafunzi hao	12	0	12
Jumla		108	96	68

3.5 Njia za Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulitumia njia mbalimbali katika kukusanya data ya utafiti ili kuweza kupata data sahihi kulingana na malengo ya utafiti husika na walengwa wa utafiti. Njia zilizotumika kukusanya data ni hojaji, mahojiano na uchunzaji darasani.

3.5.1 Hojaji au Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004), hojaji ni njia ya kukusanya data ambayo mtafiti huandika maswali na baadaye huwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia. Njia hii ilitumika kwa walimu na wanafunzi kwani mtafiti hakuwa na shaka juu ya uwezo wao wa kusoma na kuandika kwa kiswahili. Wanafunzi na walimu walipewa hojaji wakajaza papo kwa papo na kisha wakarejesha kwa ajili ya uchambuzi wa data. Njia ya hojaji ilichaguliwa kwa sababu inafaa kukusanya data katika kundi kubwa la watu na kwa muda mfupi sana hasa hojaji za papo kwa papo. Aidha, ni njia rahisi na ya haraka katika kukusanya na kuchanganua data. Data zilizopatikana kwa njia hii zilimsaidia mtafiti kujibumasiwa mawili ya utafiti ambayo yaliuliza:-

- i) Ni sababu zipi zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari?
- ii) Ni vikwazo gani vinavyokwamisha Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya Sekondari?

Kwa kuwa ni vigumu kutambua mielekeo ya wadau kupitia majibu yaliyoandikwa na watafitiwa kwenye dodoso ili kufikia hitimisho, swali la tatu lililazimu kutumia njia ya mahojiano yaliyofanyika ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa.

3.5.2 Mahojiano

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana (au simu, barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililo ainishwa. Williman (2011) ameyagawa mahojiano katika aina mbili ambazo ni, mahojiano ya ana kwa ana na mahojiano ya simu (mtandao). Ingawa njia hii inaweza kufanywa kwa njia zote hizo, mtafiti alitumia njia ya kuwahoji watafitiwa ana kwa ana kuokana na haja ya kutaka kupata mitazamo yao kwa uwazi zaidi. Njia hii ilitumika kwa walimu, wanafunzi na wazazi. Njia hii ilitumika kujibu swali la tatu lililotakakujua:-

III. Jamii ina mtazamo gani kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari?

3.5.3 Uchunzaji Darasani

Mtafiti pia alitumia mbinu ya uchunzaji. Uchunzaji ni mbinu ya kupata habari kwa kuhusisha tajriba au maarifa ya mtafiti bila kuuliza watafitiwa maswali yoyote. Uchunzaji huwa na manufaa katika mandhari ambapo watu hawapendi kujieleza kwa

kuzungumza. Pia uchunzaji unaweza kutumiwa kuthibitisha taarifa nyingine. Haya yamefafanuliwa vyema na Nkapa (1997) anaposema kwamba; Uchunzaji ukishughulikiwa vizuri, huweza kuibua mambo ya ndani ambayo njia zingine haziwezi kupata. Uchunzaji unaweza kuzalisha data asili ambayo inaweza kuaminika kinyume na ilivyo hojaji na mahojiano, data zaidi isiyotarajiwa lakini muhimu inaweza kutokea katika mazoezi ya uchunzaji. Udhaifu mkubwa sana wa uchunzaji katika utafiti ni kuwa, watafitiwa hubadili mienendo yao ya kawaida mara tu wagunduapo kuwa wanatazamwa. Licha ya udhaifu huu, mtafiti aliamua kutumia uchunzaji kwa sababu mbili kuu; uchunzaji ulimwezesha mtafiti kuchunguza na kupata taswira halisi kuhusu matumizi ya Kiswahili kwa walimu na wanafunzi. Uchunzaji uliweza kuziba mapengo ambayo yalikuwa yakizua shaka akilini mwa mtafiti, kwa kutoa ithibati kwa baadhi ya majibu ambayo yalitolewa katika hojaji ya walimu na wanafunzi pamoja na mahojiano wanafunzi, walimu na wazazi.

Mtafiti alipata fursa ya kuchunguza vielelezo viilivyokuwepo na matumizi yake na iwapo vilikuwa vimeambatanishwa maandishi katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alinuia kuelewa lugha iliyokuwa ikitawala mazungumzo baina ya walimu na wanafunzi wawapo darasani.

3.6 Vifaa vya Kukusanyia Data

Mtafiti aliandaa vifaa vya utafiti kulingana na mada na malengo ya utafiti. Vifaa hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data husika na kupata taarifa sahihi za utafiti wake.

(i) Shajara

Kifaa hiki kilimsaidia mtafiti katika kunukuu na kuhifadhi baadhi ya data za msingi kama vile taarifa za wahojiwa, data za msingi na data fuatizi katika utafiti huu.

(ii) Kinasa Sauti

Kifaa hiki kilitumika katika kunasa na kurekodi sauti wakati wote katika miktadha mbalimbali, hivyo mtafiti alikitumia kurekodi mahojiano baina yake na watafitiwa. Taarifa zilizorekodiwa zilitumika katika uchambuzi wa data katika utafiti huu.

(iii) Kompyuta

Ilitumika katika kutafutia matini kutoka katika tovuti na pia kuhifadhi taarifa mbalimbali. Data zilihifadhiwa, zilichambuliwa na kutolewa hitimisho kisha kutumika katika kuandaa ripoti ya utafiti. Pia kompyuta ilitumika kama sehemu ya maktaba tembezi.

(iii) Kinyonyi

Hiki kilitumika kuhifadhia data mbalimbali.

3.7 Uchambuzi wa Data

Kothari (2019), anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Data zilikusanywa kutoka katika vyanzo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mtafiti alitumia mkabala wa kimaielezo na kiidadi kuchambua data hizo. Data za hojaji zilichambuliwa kwa kufuata idadi na asilimia kulingana na uchaguzi wa kauli. Data mahojiano zilirekodiwa kwa kutumia kinasa sauti, kisha mtafiti alizibadili kutoka mfumo wa sauti na kuziweka kwenye maandishi kwa kuzingatia

kauli na maelezo. Uwasilishaji wa data za utafiti huu ulitumia majedwali, asilimia na maelezo ambazo ni njia rahisi kueleweka kwa mtumiaji wa utafiti.

3.8 Muhtasari

Katika sura hii ya tatu, mtafiti ameweza kueleza aina ya utafiti alioufanya, eneo ambapo utafiti wake ulifanyika, sampuli na usampulishaji yaani idadi ya watu waliohusika katika kutoa data ya utafiti na mbinu zilizotumika kuwapata watafitiwa, njia za kukusanyia data ambapo hojaji, mahojiano, na uchunzaji darasani zilitumika, vile vile vifaa vya kukusanyia data viliainishwa pamoja na mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data uliwekwa bayana.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii ni ya uwasilishaji wa data za mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Data ya utafiti huu ilikusanywa nyanjani kwa kutumia njia kuu tatu ambazo ni hojaji, mahojiano na uchunzaji darasani. Data hii ilikusanywa kutokana na sampuli ya wanafunzi wa kidato cha tatu na nne kutoka shule ya sekondari Malya, shule ya sekondari Maligisu, shule ya sekondari Mwandu na shule ya sekondari Tallo. Shule zote hizi nne zipo wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza. Vile vile data hii ilikusanywa kwa walimu wanaowafundisha wanafunzi hao pamoja na baadhi ya wazazi wa wanafunzi hao.

Uwasilishaji wa matokeo umefanyika kwa kutumia misingi ya nadharia ya hatua iliyofikiriwa iliyoasisiwa na Ajzen na Fishbein (1975). Uwasilishaji wa matokeo haya unalenga kujibu maswali ya utafiti ili kukamilisha malengo ya utafiti. Aidha, sura hii inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa data iliyochambuliwa na hoja mbalimbali za wataalamu kama zilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi za tasnifu hii. Uwasilishaji wa data umefuata mtiriko wa malengo ya utafiti, makundi ya watafitiwa na njia zilizotumika kupata data. Malengo hayo ni :-

- i) Kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.
- ii) Kubainisha vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kisitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.
- iii) Kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

4.2 Kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Lengo la kwanza la utafiti huu lilichunguza sababu zinazoshawishi matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Data za lengo hili zilikusanywa kwa kutumia hojaji zilizojazwa na walimu na wanafunzi. Uchambuzi wa data uliongozwa na nadharia ya hatua iliyofikiriwa kwa kuangalia imani waliyonayo watafitiwa kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Majibu ya watafitiwa yameoneshwa katika jedwali lifuatalo hapa chini.

4.2.1 Data za sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili zilizokusanywa uwandani kwa njia ya dodoso la walimu

Jedwali Na. 4.1 Kuonesha Majibu ya Walimu Kuhusu Sababu zinazoshawishi Matumizi ya Kiswahili Kufundishia na Kujifunzia Masomo ya Sekondari

Na	Sababu	Nakubaliana		Nakataa		Sina uhakika	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
1	Kiswahili ni lugha bora	10	62.5	4	25	2	12.5
2	Lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo	11	68.75	3	18.75	2	12.5
3	Ni lugha mama kwa wengi	7	43.75	6	37.5	3	18.75
4	Kiswahili kina msamiati toshelevu	8	50	5	31.25	3	18.75
5	Kiswahili ni lugha muhimu	9	56.25	5	31.25	2	12.5
6	Kiswahili kinaeleweka kwa urahisi	12	75	3	18.75	1	6.25

Chanzo: Data za uwandani 2023

Watafitiwa 10 (62.5%) walikubaliana na kauli ya kwanza ambayo ilisema kuwa Kiswahili ni lugha bora. Watafitiwa 4 (25%) hawakukubaliana na kauli hiyo na watafitiwa 2 (12.5%) hawakuwa na uhakika na kauli ya kuwa Kiswahili ni lugha bora.

Kauli ya kuwa lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo, iliungwa mkono na watafitiwa 11 (68.75%) huku watafitiwa 3 (18.75%) wakipinga, ilhali 2 (12.5%) wasijue la kusema. Yamkini idadi kubwa iliyokubaliana kuwa lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo, ndiyo hutumia Kiswahili mara kwa mara katika mawasiliano yao.

Watafitiwa waliuzwa watoe uamuzi wao kuhusu Kiswahili kuwa lugha mama kwa walio wengi, watafitiwa 7 (43.75%) walikiri kuwa Kiswahili ni lugha mama kwa walio wengi. Watafitiwa 6 (37.5%) walikataa na watafitiwa 3 (18.75%) hawakuwa na uhakika juu ya kauli hiyo.

Kauli ya kuwa Kiswahili kina msamiati toshelevu, liliungwa mkono na jumla ya watafitiwa 8 (50%) huku 5 (31.25%) walipinga, ilhali 3 (18.75%) walikosa uamuzi mahsusi.

Watafitiwa walihitajika kutoa msimamo wao kuhusiana na kauli kuwa, Kiswahili ni lugha muhimu. Watafitiwa 9 (56.25%) walikubaliana, watafitiwa 3 (31.25%) walikataa na huku 2 (12.5%) wakikosa msimamo dhabiti.

Walimu walitakiwa kutoa msimamo wao kuhusu madai ya kuwa Kiswahili kinaeleweka kwa urahisi. Watafitiwa 12 (75%) walikubaliana na kauli hii, ilhali 3 (18.75%) walikataa na watafitiwa 1 (6.25%) hakuwa na uhakika na kauli hii.

Kwa ujumla wastani wa walimu 10 (62.25%) ya watafitiwa wanashawishika na sababu zilizotolewa kukifanya Kiswahili kitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari, walimu 4(25%) hawashawishiki na sababu hizo na walimu 2(12.5%) hawana uhakika wa sababu zilizoelezwa.

4.2.2 Data kuhusu sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia zilizokusanywa uwandani kwa njia ya dodoso la wanafunzi

Jedwali Na. 4.2 Kuonesha Majibu ya Wanafunzi Kuhusu Sababu zinazoshawishi Matumizi ya Kiswahili Kufundishia Na Kujifunzia Masomo ya Sekondari

Na	Sababu	Nakubaliana		Nakataa		Sina uhakika	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
1	Kiswahili ni lugha bora	63	78.75	9	11.25	8	10
2	Lugha ya Kiswahili hutawala azungumzo	59	73.75	14	17.5	7	8.75
3	Ni lugha mama kwa wengi	48	60	21	26.25	11	13.75
4	Kiswahili kina msamiati toshelevu	53	66.25	17	21.25	10	12.5
5	Kiswahili ni lugha muhimu	47	58.75	24	30	9	11.25
6	Kiswahili kinaeleweka kwa urahisi	69	86.25	8	10	3	3.75

Chanzo: Data za uwandani 2023

Katika kauli ya kwanza, watafitiwa 63 (78.75%) walikubali kuwa Kiswahili ni lugha bora ya kufundishia, watafitiwa 9 (11.25%) walikana, huku 8 (10%) wakikosa uhakika wa jawabu. Aidha matokeo hayo yanaonyesha kuwa ufaafu wa lugha hii ni

bayana, kwa sababu kulikuwa na tofauti kubwa sana kati ya waliounga mkono na walioshindwa kukubaliana na kauli hii.

Katika kauli ya pili iliyodahili kuwa Kiswahili hutawala mazungumzo, watafitiwa 59 (73.75%) walikubali huku 14 (17.5%) wakikana na mtafitiwa 7 (8.75%) walikosa msimamo juu ya kauli hii. Matokeo ya kauli hii yanadhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili hutumiwa na wengi katika eneo la utafiti.

Dhana kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha mama, iliungwa mkono na watafitiwa 48 (60%), watafitiwa 11 (13.75%) hawakuwa na msimamo, waliosalia 21 (26.25%) walikana. Tarakimu hizi zinaonyesha kuwa watafitiwa wengi wanakubaliana kuwa Kiswahili ni lugha mama, idadi inayopinga kauli hii inaashiria kuwa wanatambua lugha zao za Kienyeji kama lugha mama.

Wanafunzi walitarajiwa kutoa mchango wao kuhusiana na kauli kuwa lugha ya Kiswahili ina msamiati toshelevu. Kauli hii ya msamiati kwa kiwango hiki cha sekondari ni muhimu na ndiyo hujenga msingi wa lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 53 (66.25%) walikubaliana na kauli hiyo, watafitiwa 17 (21.25%) waliikataa na watafitiwa waliosalia 10 (12.5%) hawakujua la kusema. Matokeo haya yanaonesha kuwa Kiswahili kina msamiati unaoweza kotosheleza matakwa ya watumiaji wake.

Kwa upande mwingine, walipoulizwa maoni yao kuhusiana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, watafitiwa 47 (58.75%) walikubali kuwa ni lugha muhimu, watafitiwa 24 (30%) walikataa ilhali 9 (11.25%) hawakuwa na uhakika wa kauli ya mtafiti. Idadi kubwa ya watafitiwa kwenye hojaji ilikubaliana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, hili lilitokana na matumizi yake katika mandhari ya shuleni na nyumbani.

Wale waliopinga kuwa lugha ya Kiswahili sio muhimu ni wale ambao hawakupenda lugha ya Kiswahili.

Katika kauli ya mwisho, wahojiwa waliulizwa sababu ya kuhusiana na Kiswahili kueleweka kwa urahisi kama inaweza kuwa sababu ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Wahojiwa 69 (86.25%) walikubaliana na mtafiti, wahojiwa 8 (10%) walikataa na 3 (3.75%) hawakuwa na uhakika.

Kwa ujumla watafitiwa 57(71.25%) wamekubaliana na sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili, watafitiwa 15(18.75%) wamezikataa sababu hizo na watafitiwa 8(10%) hawana uhakika na sababu yoyote ile.

Hivyo basi, data iliyokusanywa kwa walimu na data iliyokusanywa kwa wanafunzi zinaashiria idadi kubwa ya watafitiwa wanakubaliana na sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili. Imani yao katika lugha ya Kiswahili kama lugha itakayowaletea manufaa ni kubwa. Hivyo maoni yao yanakubaliana na nadharia ya hatua iliyofikiriwa ambayo imeeleza kuhusu masula ya imani kama kichocheo cha mtu kutaka kukubaliana na tabia fulani. Maoni yao yanakwenda sanjari na mitazamo ya wataalamu waliotafiti kuhusu lugha ya kufundishia kama vile Tikolo (2012) aliyeeleza kuwa uelewa wa wanafunzi wa lugha aliyoizoea katika makuzi yake inaweza kuwa ndiyo msingi wa ujifunzaji mzuri wa baadae, pale anapounganisha na ujuzi wa mwalimu wake. Zaidi ya hapo, Senkoro (2004) katika utafiti wake alieleza kuwa ujifunzaji na ufundishaji unatakiwa uwe katika lugha inayoeleweka vizuri kwa walimu na wanafunzi.

4.3 Kubainisha vikwazo vinavyokwamisha Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Lengo la pili la utafiti huu lilichunguza vikwazo vinavyoikabili Lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Uchambuzi wa data katika lengo hili ulizingatia msingi wa nadharia ya hatua iliyofikiriwa kwa kuangazia nia au kusudio la mtu la kutaka kubadili hali fulani ili kunufaika zaidi. Data zilizowasilishwa zilipatikana kwa njia ya hojaji iliyojazwa na walimu na wanafunzi.

4.3.1 Data za Vikwazo Vinavyokabili Kiswahili Zilizokusanywa Uwandani kwa Njia ya Dodoso la Walimu

Jedwali Na. 4.3 Kuonesha Majibu ya Walimu Kuhusu Dodoso la vikwazo vinavyoikabili Lugha ya Kiswahili Isitumike katika Kufundisha na Kujifunza Masomo ya Sekondari

Na.	Vikwazo vya Kiswahili kutotumika	Nakubali ana sana	Nakubali ana	Sina uhakika	Nakataa	Nakataa Kabisa
1	Kulegalega kwa sheria ya lugha nchini Tanzania	8	5	0	2	1
2	Udhaifu katika asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.	7	5	1	2	1
3	Kiswahili kutokuwa na hadhi	9	4	1	1	1
4	Kulegalega kwa sera ya lugha	5	6	1	2	2
5	Msukumo mdogo kutoka kwa viongozi wa kisiasa	3	6	2	3	2

Chanzo: Data za uwandani 2023

Swali la kwanza lilikuwa ni kulegalega kwa sheria ya lugha nchini Tanzania kikwazo kwa lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari? Takwimu za wahojiwa waliojaza dodoso kuhusu swali hili walikuwa walimu 16. Wahojiwa 8 (50%) walikubaliana sana na mtafiti, wahojiwa 5 (31.25%) walikubaliana na mtafiti, hakuna wahojiwa waliokuwa hawana uhakika na swali la mtafiti, wahojiwa 2 (12.5%) walikataa swali la mtafiti na mhojiwa 1 (6.25%) alikaa kabisa swali mtafiti. Kwa takwimu hizi, wahojiwa waliokubaliana sana na kukubaliana na mtafiti ni (81.25%) wakati watafitiwa waliokataa na kukataa kabisa swali la mtafiti ni (18.75%) na hakukuwa na mhojiwa hata mmoja alikuwa hana uhakika na swali la mtafiti. Kwa takwimu hizi za waliokubaliana na swali la mtafiti upo udhaifu mkubwa wa sheria ya matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania.

Swali la pili lilikuwa ni Udhaifu katika asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahilini kikwazo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari? Walimu 16 Walijibu ambapo 7 (43.75%) walikubaliana sana na swali la mtafiti, wahojiwa 5 (31.25%) walikubaliana na mtafiti, mhojiwa 1 (6.25%) hakuwa na uhakika na swali la mtafiti, wahojiwa 2 (12.5%) walikataa na mhojiwa 1 (6.25%) alikataa kabisa swali la mtafiti. Mtafiti alionesha takwimu za waliokubaliana sana na walikubaliana na swali la mtafiti kuwa ni 75% ya wahojiwa wote wakati waliokataa na kukataa kabisa ni 18.75% ya wahojiwa wote na wahojiwa ambao hawakuwa na uhakika na swali la mtafiti ni 6.25%. Kwa takwimu hizi kutoka uwandani mtafiti aliweka wazi kuwa upo udhaifu mkubwa wa asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza Kiswahili.

Swali la tatu lilikuwa ni Kiswahili kutokuwa na hadhini kikwazo kwa lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia masomo ya sekondari? Mtafiti aligawa hojaji kwa walimu 16 ili wakubaliane au wapinge kauli ya mtafiti. Katika data zilizokusanywa uwandani kwa kutumia hojaji zilionesha kuwa wahojiwa 9 (56.25%) walikubaliana sana na swali la mtafiti, wahojiwa 4 (25%) walikubaliana na mtafiti, mhojiwa 1 (6.25%) hakuwa na uhakika wa swali la mtafiti, mhojiwa 1 (6.25%) alikataa swali la mtafiti na mhojiwa 1 (6.25%) alikataa kabisa swali la mtafiti. Takwimu hizi za uwandani, zilionesha watafiti waliokubaliana sana na waliokubaliana na swali la mtafiti ni 81.25% wakati wahojiwa waliokataa na kukataa kabisa ni 12.5% na wahojiwa walionekana kutokuwa na uhakika na swali la mtafiti 6.25%. Kwa data hizi kutoka uwandani, ilibainisha wazi kuwa hadhi ya Kiswahili ni kikwazo kufundishia masomo ya sekondari.

Swali la nne lilikuwa ni kulegalega kwa sera ya lughani kikwazo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari? wahojiwa 16 walijaza hojaji zao ambapo wahojiwa 5 (31.25%) walikubaliana sana na swali la mtafiti, watafitiwa 6 (37.5%) walikubaliana na swali la mtafiti, mhojiwa 1 (6.25%) alisema hana uhakika na swali la mtafiti, wahojiwa 2 (12.5%) walikataa swali la mtafiti na watafitiwa 2 (12.5%) walikataa kabisa swali la mtafiti. Kwa takwimu hizi kutoka uwandani zilionesha kuwa waliokubaliana sana na kukubaliana na swali la mtafiti ni 68.75% wakati waliokataa na kukataa kabisa swali la mtafiti ni 25% na wahojiwa ambao walionekana kutokuwa na uhakika na swali la mtafiti ni 6.25%. Kwa takwimu hizi, ilibainika wazi kuwa kulegalega kwa sera ya lugha ni kikwazo kwa Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Swali la tano lilikuwa ni msukumo mdogo kutoka kwa viongozi wa kisiasa ni kikwazo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari? Mtafiti aligawa hojaji kwa walimu 16 ambapo watafitiwa 3 (18.75%) walikubaliana sana na swali la mtafiti, wahojiwa 6 (37.5%) walikubaliana na swali la mtafiti, watatiwa 2 (12.5%) hawakuwa na uhakika wa swali la mtafiti, watafitiwa 3 (18.75%) walikataa swali ya mtafiti na watafitiwa 2 (12.5%) walikataa kabisa swali la mtafiti. Kwa data hizi kutoka uwandani zilizokusanywa na hojaji zilionesha waliokubaliana sana na waliokubaliana na swali la mtafiti ni 56.25% wakati waliokataa na kukataa kabisa ni 31.25% na watafitiwa ambao walionesha kutokuwa na uhakika na swali la mtafiti ni 12.5%. Kwa takwimu hizi, upo msukumo mdogo kwa viongozi wa kisiasa kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Kwa ujumla wastani wa walimu 11 (62.5%) ya watafitiwa wanakubaliana na kuwepo kwa vikwazo vinavyoifanya lugha ya Kiswahili isitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari na 4 (25%) hawakubaliani na vikwazo hivyo na mwalimu 1 (6.25%) hakuwa na uhakika kuhusu uwepo au kutokuwepo kwa vikwazo. Tafsiri ya data hii ni kuwa walimu wengi wana nia ya kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia masomo ya sekondari isipokuwa wanashindwa kulitekeleza hilo kutokana na vikwazo mbalimbali ambavyo viko nje ya uwezo wao.

4.3.2 Data za Vikwazo Vinavyokabili Kiswahili Zilizokusanywa Uwandani kwa Njia ya Dodoso ya Wanafunzi

Jedwali Na. 4.4 Kuonesha Majibu ya Wanafunzi Kuhusu Dodoso la vikwazo vinavyoikabili Lugha ya Kiswahili Isitumike katika Kufundisha na Kujifunza Masomo ya Sekondari

Na.	Vikwazo vyaa Kiswahili kutotumika.	Nakubali ana sana	Nakubali ana	Sina uhakika	Nakataa	Nakataa Kabisa
1	Kulegalega kwa sheria ya lugha nchini Tanzania	23	36	3	9	8
2	Udhaifu katika asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.	25	37	7	4	7
3	Kiswahili kutokuwa na hadhi	32	37	3	5	3
4	Kulegalega kwa sera ya lugha	19	43	4	6	8
5	Msukumo mdogo kutoka kwa viongozi wa kisiasa	22	35	7	7	8

Chanzo: Data za uwandani 2023

Katika sehemu hii, mtafiti alichanganua maswali ya hojaji ya wanafunzi kuhusiana na vikwazo vinavyozuia lugha ya Kiswahili isitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Mtafiti alichambua data kwa kuonesha waliokubaliana na wasiokubaliana na kauli za mtafiti.

Swali la kwanza lilikuwa niKulegalega kwa sheria ya lugha nchini Tanzaniani kiwazo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kujifunzia masomo ya sekondari? Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 80 waliopewa hojaji na mtafiti ambapo watafitiwa 23

(28.75%) walikubaliana sana na mtafiti, watafitiwa 36 (45%) walikubaliana na mtafiti, watafitiwa 3 (3.75%) hawakuwa na uhakika na kauli ya mtafiti, watafitiwa 9 (11.25%) walikataa kauli ya mtafiti na watafitiwa 8 (10%) walikataa kabisa kauli ya mtafiti. Takwimu za waliokubaliana sana na kukubaliana na mtafiti ni 68.75% wakati walikataa na kukataa kabisa ni 21.25% na ambao hawakuwa na uhakika na kauli ya mtafiti ni 3.75%. Kwa takwimu hizi kutoka uwandani zilizokusanywa na hojaji, ilibainika wazi kuwa sheria ya lugha inalegalega.

Swali la pili lilikuwa ni udhaifu wa asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili ni kikwazo kuhusu kutumia lugha ya Kiswahili kujifunzia masomo ya sekondari? Mtafiti aligawa hojaji kwa wanafunzi 80 ambapo wahojiwa 25 (31.25%) walikubaliana sana na mtafiti, wahojiwa 37 (46.25%) walikubaliana na mtafiti, wahojiwa 7 (8.75%) hawakuwa na uhakika na kauli ya mtafiti, wahojiwa 4 (5%) walikataa kauli ya mtafiti na wahojiwa 7 (8.75%) walikataa kabisa. Takwimu zilizotoka uwandani zilionesha kwa waliokubaliana sana na waliokubaliana na mtafiti ni 77.5% wakati waliokataa na kukataa kabisa ni 13.75% na walionekana kutokuwa na uhakika na kauli ya mtafiti ni 8.75%. Kwa data hojaji zilizotoka uwandani, ilibainika wazi kuwa upo udhaifu mkubwa wa asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza Kiswahili.

Swali la tatu lilikuwa ni Kiswahili kutokuwa na hadhi ni kikwazo kuhusu kutumika kujifunzia masomo ya sekondari?. Mtafiti aligawa hojaji kwa wanafunzi 80 ambapo wahojiwa 32 (40%) walikubaliana sana na mtafiti, wahojiwa 37 (46.25%) walikubaliana na mtafiti, mhojiwa 3 (3.75%) hakuwa na uhakika, wahojiwa 5 (6.25%) walikataa na wahojiwa 3 (3.75%) walikataa kabisa. Kwa takwimu za

uwandani zilizokusanywa na hojaji zilionesha kuwa waliokubaliana sana na waliokubaliana na mtafiti ni 86.25% wakati waliokataa na waliokataa kabisa ni 10% na ambao hawakuwa na uhakika ni 3.75%. Mtafiti aliweka wazi kuwa kwa data za uwandani Kiswahili kilionekana hakina hadhi.

Swali la nne lilikuwa ni Kulegalega kwa sera ya lughani kikwazo kwa lugha ya Kiswahili kutumika kujifunzia masomo nya sekondari? Mtafiti aligawa hojaji kwa wanafunzi 80 ili wapinge au wakubaliane na swali la mtafiti. Matokeo ya hojaji kutoka uwandani yalionesha kuwa wahojiwa 19 (23.75%) walikubaliana sana na mtafiti, wahojiwa 43 (53.75%) walikubaliana na mtafiti, wahojiwa 4 (5%) hakuwa na uhakika, wahojiwa 6 (7.5%) walikataa na wahojiwa 8 (10%) walikataa kabisa. Kwa takwimu hizi kutoka uwandani zilionesha kuwa waliokubaliana sana na waliokubaliana na mtafiti ni 77.5% wakati waliokataa na kukataa kabisa ni 17.5% na ambao hawakuwa na uhakika ni 5%. Mtafiti aliweka wazi kuwa sera ya lugha ni kikwazo.

Swali la tano lilikuwa ni msukumo mdogo kutoka kwa viongozi wa kisiasa ni kikwazo kwa lugha ya Kiswahili kujifunzia masomo ya sekondari?. Mtafiti aligawa hojaji kwa wanafunzi 80 ambapo wahojiwa 22 (27.5%) walikubaliana sana na mtafiti, wahojiwa 35 (43.75%) walikubaliana na mtafiti, wahojiwa 8 (10%) hakuwa na uhakika, wahojiwa 7 (8.75%) walikataa na wahojiwa 8 (10%) walikataa kabisa. Takwimu za uwandani zilizokusanywa na hojaji zilionesha kuwa waliokubaliana sana na waliokubaliana na mtafiti ni 71.25% wakati waliokataa na waliokataa kabisa ni 18.75% na ambao hawakuwa na uhakika ni 10%. Kwa uchambuzi uliofanywa na

mtafiti ulibainisha wazi kuwa msukumo mdogo wa viongozi wa kisiasa ni kikwazo kikubwa cha matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Kwa ujumla wastani wa wanafunzi 62 (77.5%) ya watafitiwa wanakubaliana na vikwazo vinavyoifanya lugha ya Kiswahili isitumike kujifunzia masomo ya sekondari, wanafunzi 13(16.25%) hawakubaliani na vikwazo hivyo na wanafunzi 5(6.25%) hawana uhakika kuhusu uwepo au kutokuwepo kwa vikwazo.

Data iliyokusanywa kwa walimu na wanafunzi kupitia hojaji imeashiria kuwa walimu na wanafunzi wengi wanaufahamu wa kutosha juu ya vikwazo vinavyoifanya lugha ya Kiswahili isitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Nia yao ya kuweka wazi vikwazo hivyo ni kutaka hatua zichukuliwe ili kuondoa vikwazo hivyo. Maoni haya yanakubaliana na nadharia ya hatua iliyofikiriwa inayozugumzia ari ya mtu kukusudia au kunuia kufanya jambo ambalo anaona litaleta manufaa kwake na kwa jamii. Senkoro(2004) anatoa hoja kuwa, pamoja na jitihada za serikali kuchochea kuanzishwa kwa vyombo rasmi vya kuendeleza lugha ya Kiswahili, jitihada hizo hazuandamana na utungaji wa sheria ya kutilia mkazo utekelezaji wa matakwa na mahitaji ya hadhi hiyo, ambayo ni pamoja na kufundishia elimu kwa viwango vyote.

4.4 Kutathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Lengo la tatu la utafiti huu lilijikita katika kutathmini mtazamo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Wadau waliohusishwa ni walimu, wanafunzi na wazazi. Njia ya mahojiano ilitumika kupata

taarifa kwa watafitiwa. Uchambuzi wa data hii uliongozwa na nadharia ya hatua iliyofikiriwa katika kutathmini hali na mtazamo wa watafitiwa kuhusiana na matumizi ya Kiswahili. Uwasilishaji wa data umezingatia makundi kwa kuanza na mahojiano ya walimu, wanafunzi na wazazi.

4.4.1 Data ya mtazamo wa walimu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Jedwali Na. 4.5 Kuonesha majibu ya walimu ya mahojiano yaliyofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Na.	Maswali	Majibu	
1.	Unatumia lugha ipi kati ya hizi katika mawasiliano yako ya mara kwa mara? a. Kisukuma b. Kiswahili c. Kiingereza d. Lugha nyingine	Lugha	Idadi ya uchaguzi/marudio
		Kisukuma	2
		Kiswahili	10
		Kiingereza	0
		Lugha nyingine	4
2.	Una maoni yapi kuhusu lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Chagua kauli moja kati ya hizi? a) Lugha ya Kiswahili inafaa sana b) Lugha ya Kiswahili inafaa c) Lugha ya Kiswahili haifai sana d) Lugha Kiswahili haifai e) Sina uhakika	kauli	idadi ya uchaguzi/marudio
		Inafaa sana	4
		inafaa	3
		Haifai sana	2
		haifai	4
		Sina uhakika	3
3.	Eleza kwa kifupi sababu za uchaguzi wako katika swali la 2?	Majibu yapo chini kwenye maelezo	

Chanzo: Data za uwandani 2023

Katika mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa (walimu). Mtafiti aliuliza maswali matatu ili kuweza kupata mielekeo juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Swali la kwanza lilimtaka mtafitiwa achague lugha anayopendelea kuitumia katika mawasiliano yake ya kawaida. Jumla ya watafitiwa waliohojiwa ilikuwa 16, watafitiwa 2(12.5%) walichagua lugha ya kisukuma, watafitiwa 10(62.5%) walichagua lugha ya Kiswahili na watafitiwa 4(25%) walichagua lugha nyingine. Hakuna mtafitiwa aliyechagua lugha ya Kiingereza kuwa anaitumia katika mawasiliano yake ya kawaida.

Swali la pili lilimtaka mtafitiwa atoe maoni yake kuhusu pendekezo la Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia masomo ya sekondari. Mtafiti alitumia kauli tano ambazo alimtaka mtafitiwa achague kauli moja kutokana na mtazamo wake. Watafitiwa 4(25%) walichagua kauli iliyosema inafaaa sana, watafitiwa 3(18.75%) walichagua kauli ya inafaa, watafitiwa 2(12.5) walichagua kauli iliyosema haifai kabisa, watafitiwa 4(25%) walichagua kauli ya haifai na watafitiwa 3(18.5) hawakuwa na uhakika.

Swali la tatu lilimtaka mtafitiwa kueleza sababu za maoni yake katika swali la 2. Mwalimu kutoka shule ya sekondari Malya alisema Kiswahili kinafaa sana alisema *“...aaaah!... Kiswahili ni lugha rahisi k kufundishia na kujifunziani lugha ambayo inafahamika vizuri kwa walimu, wanafunzi na hata katika jamii”*. Naye Mwalimu kutoka Maligisu aliyehagua kauli kuwa Kiswahili kinafaa sana alisema *“...ninavyofikiri mimi....uelewa,ubunifu na udadisi unajengwa kwa kutumia lugha*

rahisi na inayofahamika.....ndiyo maana nchi kama China wameeendelea kwa sababu wanatumia lugha yao wenyewe.....hata sisi tukitumia Kiswahili tunaweza kuyafikia mafanikio hayo’’

Mwalimu kutoka shule ya sekondari Mwandu aliyechagua kuwa lugha ya Kiswahili haifai sana alisema “....Mmmm.....Lugha ya Kiswahili haijafikia kiwango cha kushindana na lugha za kimagharibi.....kuamua kutumia lugha hii ya Kiswahili kutasababisha wataanzania washindwe kushindana katika soko la ajira hasa katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia’ Mwalimu kutoka shule ya sekondari Tallo aliongeza kuwa “....pamoja na kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa lakini matumizi yake katika kufundishia yanaathari kubwa katika masomo ya sayansi.....hakuna misamiati ya kutosha kuelezea dhana za kisayansi na hata hiyo michachache inayoletwa ni migumu’’

4.4.2 Data ya mtazamo wa wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Jedwali Na. 4.6 Kuonesha majibu ya wanafunzi ya mahojiano yaliyofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Na.	Maswali	Majibu	
1.	Unatumia lugha ipi kati ya hizi katika mawasiliano yako ya mara kwa mara? a. Kisukuma b. Kiswahili c. Kiingereza d. Lugha nyingine	Lugha	Idadi ya uchaguzi/marudio
		Kisukuma	21
		Kiswahili	16
		Kiingereza	0
		Lugha nyingine	3
2.	Una maoni yapi kuhusu lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Chagua kauli moja kati ya hizi? a. Lugha ya Kiswahili inafaa sana b. Lugha ya Kiswahili inafaa c. Lugha ya Kiswahili haifai sana d. Lugha Kiswahili haifai e. Sina uhakika	kauli	idadi ya uchaguzi/marudio
		Inafaa sana	12
		inafaa	14
		Haifai sana	5
		haifai	7
		Sina uhakika	4
3.	Eleza kwa kifupi sababu za uchaguzi wako katika swali 2?	Majibu yapo chini kwenye maelezo	

Chanzo: Data za uwandani 2023

Katika mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa (wanafunzi).Mtafiti aliuliza maswali matatu ili kuweza kupata mtazamo juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Swali la kwanza lilitaka mtafitiwa achague lugha anayopendelea kuitumia katika mawasiliano yake ya kawaida.Jumla ya watafitiwa waliohojiwa ilikuwa 40, watafitiwa 21(52.5%) walichagua lugha ya Kisukuma, watafitiwa 16(40%) walichagua lugha ya Kiswahili na watafitiwa 3(7.5%) walichagua lugha nyingine. Hakuna mtafitiwa aliyechagua lugha ya Kiingereza kuwa anaitumia katika mawasiliano yake ya kawaida.

Swali la pili lilimtaka mtafitiwa atoe maoni yake kuhusu pendekezo la Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia masomo ya sekondari. Mtafiti alitumia kauli tano ambazo alimtaka mtafitiwa achague kauli moja kutokana na mtazamo wake. Watafitiwa 12(30%) walichagua kauli iliyosema inafaaa sana, watafitiwa 14(35%) walichaguakauli ya inafaa, watafitiwa 5(12.5) walichagua kauli iliyosema haifai kabisa, watafitiwa 7(17.5%) walichagua kauli ya haifai na watafitiwa 4(10%) hawakuwa na uhakika.

Swali la tatu lilimtaka mtafitiwa kueleza sababu za maoni yake katika swali la 2. Mwanfunzi kutoka Shele ya sekondari Maligisu alisema “*...lugha ya kiswhili inafaa sana kwa sababu nailewa vizuri....lugha ya kiingerezani ya kukariri maneno bila kuyaelewa....labda nifafanuliwe kwa Kiswahili au nitumie kamusi*”.Naye mwanafunzi kutoka shule ya sekondari Malya alisema “*ni bora tu kufundishwa kwa Kiswahili.....lugha ya Kiingereza ni ngumu sana*”

Mwanafunzi kutoka shule ya sekondari Tallo alisema “....sikubaliani na matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa sababu.....siyo lugha ya kimataifa”.Mwanafunzi mwingine kutoka shule ya sekondari Tallo aliongeza kuwa “lugha ya Kiswahili haikupeleki popote.....hata huko chuo kikuu wanafundishwa kwa lugha ya kiingereza”

4.4.3 Data ya mtazamo wa wazazi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Jedwali Na. 4.7 kuonesha majibu ya wazazi ya mahojiano yaliyofanyika kuhusu mtazamo wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari

Na.	Maswali	Majibu	
		lugha	Idadi ya uchaguzi/marudio
1.	Unatumia lugha ipi kati ya hizi katika mawasiliano yako ya mara kwa mara? a) Kisukuma b) Kiswahili c) Kiingereza d) Lugha nyingine	Kisukuma	8
		Kiswahili	4
		Kiingereza	0
		Lugha nyingine	0
2.	Una maoni yapi kuhusu lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Chagua kauli moja kati ya hizi? a. Lugha ya Kiswahili inafaa sana b. Lugha ya Kiswahili inafaa c. Lugha ya Kiswahili haifai sana d. Lugha Kiswahili haifai e. Sina uhakika	kauli	Idadi ya uchguzi/marudi
		Inafaa sana	3
		Inafaaa	3
		Haifai sana	1
		Haifai	2
		Sina hakika	3
3.	Eleza kwa kifupi sababu za uchaguzi wako katika swali 2?	Majibu yapo chini kwenye maelezo	

Chanzo: Data za uwandani 2023

Katika mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na watafitiwa (wazazi). Mtafiti aliuliza maswali matatu ili kuweza kupata mtazamo juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Swali la kwanza lilimtaka mtafitiwa achague lugha anayopendelea kuitumia katika mawasiliano yake ya kawaida. Jumla ya watafitiwa waliohojiwa ilikuwa 12, watafitiwa 8 (66.7%) walichagua lugha ya Kisukuma, watafitiwa 4(33.3%) walichagua lugha ya Kiswahili na. Hakuna mtafitiwa aliyechagua lugha ya Kiingereza na lugha nyingine kuwa anaitumia katika mawasiliano yake ya kawaida.

Swali la pili lilimtaka mtafitiwa atoe maoni yake kuhusu pendekezo la Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia masomo ya sekondari. Mtafiti alitumia kauli tano ambazo alimtaka mtafitiwa achague kauli moja kutokana na mtazamo wake. Watafitiwa 3(25%) walichagua kauli iliyosema inafaaa sana, watafitiwa 3(25%) walichaguakauli ya inafaa, mtafitiwa 1(8.3%) walichagua kauli iliyosema haifai kabisa, watafitiwa 2(16.7%) walichagua kauli ya haifai na watafitiwa 3(25%) hawakuwa na uhakika.

Swali la tatu lilimtaka mtafitiwa kueleza sababu za maoni yake katika swali la 2.Mzazi kutoka Malya alisema “*....oooh!....Kiswahili kinafaa.....kule sekondari Kiingereza kinawashinda ndiyo maana wanafunzi wengi wa sekondari wanafeli*”. Mzazi mwingine kutoka Mwandu alisema “*....wakitumia Kiswahili wanafunzi wengi wataipenda shule.....kuna mwanangu aliicha shule kwa kuogopa adhabu za kuongea Kiswahili shuleni*”.Mzazi kutoka Maligisu alisema “*.....mtu mwenye elimu*

lazima azungumze Kiingereza.....wakifundishwa kwa Kiswahili hawataweza kuzungumza Kiingereza.

Kupitia njia ya mahojiano kwa walimu, wanafunzi na wazazi imebainika kuwa Kiswahili kinatumika sambamba na lugha za asili katika mawasiliano ya kawaida. Aghalabu Kiingereza hutumika maeneo rasmi tu. Hali kadhalika, watafitiwa wengi wamekuwa na mtazamo chanya wa matumizi Kiswahili kufundishia na kujifunzia. Hii ni kutokana na umuhimu na matarajio makubwa waliyonayo endapo lugha hii itapewa hadhi hiyo. Maoni ya watafitiwa yanawiana na misingi ya nadharia ya hatua iliyofikiriwa kuhusu suala la kuwa na mtazamo hasi au chanya. Mtazamo huu chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili unaafikiana na maoni ya Simala (2006) aliyedai kuwa lugha ya Kiswahili ina utajiri wa msamiati wa kufundishia na haina tatizo kama wengi wanavyoamini kuwa imepungukiwa msamiati faafu kwa masomo ya sayansi.

4.5 Data Zilizokusanywa kwa njia ya Uchunzaji Darasani

Mtafiti alitumia njia hii kuthibitisha baadhi ya data zilizokusanya kwa hojaji na mahojiano. Njia hii ilimwezesha mtafiti kupata mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

Kupitia uchunzaji darasani mtafiti alibaini uwepo wa matumizi ya Kiswahili na Kiingereza katika vielelezo mbalimali. Mtafiti aliona orodha iliyoandikwa “inventory sheet” ila vipengele vyake vilijazwa kwa lugha ya Kiswahili. Vifaa hivyo viliandikwa meza, viti na taa ambapo kipengele cha idadi nacho kilijazwa kwa Kiswahili. Vile vile ratiba ya masomo ya kidato cha tatu katika shule zilizotafitiwa

ilibainika baadhi ya vipengele Kama somo, kipindi na muda viliandikwa kwa lugha ya Kiswahili wakati masomo yenyewe yaliandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mtafiti alibaini katika baadhi ya shule, ratiba za usafi ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Pia alibaini uwepo wa taarifa ya matokeo katika shule moja wapo iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Pia walimu waliokwenda kumtambulisha mtafiti kwa wanafunzi darasani walitumia lugha ya Kiswahili.

Mbinu hii ya uchunzaji darasani ilibaini wazi kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayotawala mazungumzo, lugha muhimu na inaeleweka kiurahisi kwa wanafunzi wote. Alibaini pia lugha ya Kiingereza haisimami pekee katika miktadha mbalimbali hadi ichanganywe na lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka.

4.6 Muhtasari

Sura hii imewasilisha na imechambua data za utafiti. Data zimewasilishwa kulingana na malengo na njia zilizotumika kuzikusanya. Uchambuzi wa data umeongozwa na nadharia ya hatua iliyofikiriwa.

SURA YA TANO

MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo, mapendekezo na hitimisho la utafiti huu. Sehemu ya kwanza inahusu matokeo na mjadala, sehemu ya pili inahusu mapendekezo kwa tafiti zijazo na mapendekezo ya jumla ya utafiti huu na sehemu ya tatu ni hitimisho la utafiti huu kwa ujumla.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inatoa matokeo ya utafiti baada ya zoezi la kuwasililisha na kuchambua data za utafiti huu. Uwasilishaji wa matokeo umezingatia malengo ya utafiti.

Lengo la kwanza la utafiti lilitaka kubainisha sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundisha na kujifunza masomo ya sekondari sababu hizo ni Kiswahili kuwa lugha bora, Kiswahili kutawala mazungumzo, Kiswahili kuwa lugha mama kwa walio wengi, Kiswahili kuwa na msamiati toshelevu, Kiswahili ni lugha muhimu na Kiswahili kueleweka kwa urahisi. Utafiti umeonesha kuwa walimu na wanafunzi wanaunga mkono hoja kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kufundishia masomo ya sekondari. Msanjila na wenzake (2011) walishauri kwamba, kutumia lugha sahihi katika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu ni zaidi ya kuwasaidia wanaojifunza kwa sababu huendeleza pia vipaji vyao, na kubwa zaidi lugha hiyo huendelezwa ili kukabili mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayojitokeza.

Lengo la pili lilibainisha vikwazo vinavyokwamisha lugha ya Kiswahili na isitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Utafiti umebaini kuwepo kwa vikwazo mbalimbali ambavyo vimeidhofisha lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Vikwazo hivyo ni pamoja na kulegalega kwa sheria ya lugha nchini Tanzania, udhaifu katika asasi na vyombo vya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili, Kiswahili kutokuwa na hadhi, kulegalega kwa sera ya lugha na msukumo mdogo kutoka kwa viongozi wa kisiasa.

Lengo la tatu lilitathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Utafiti umebaini kuwepo kwa mtazamo chanya wa matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Mtazamo chanya wa matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sekondari ni mahitaji ya msingi ili kuwezesha walimu na wanafunzi kutoa na kupokea maarifa, stadi na ujuzi bila kuwa na kikwazo cha lugha.

5.3 Mapendekezo

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa Serikali ione umuhimu wa kuipa hadhi lugha ya Kiswahili itumike kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Lugha ya Kiingereza ifundishwe ikiwa na mlengo wa kukuza stadi za mawasiliano tu na isiwe lugha ya kufundishia masomo ya sekondari.

5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulijikita katika mtazamo kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari na mifano imetoka Wilaya ya Kwimba Mkoa wa Mwanza. Utafiti huu umefanikiwa kupata mtazamo chanya uliopo kwa walimu,

wanafunzi na wazazi wakieleza umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Utafiti huu unapendekeza tafiti nyingine zifanyike katika maeneo mengine ili kulinganisha matokeo ya tafiti hizo na utafiti huu. Pili, mtafiti hakumaliza kubainisha matatizo yote ya lugha ya kufundishia na kujifunzia katika mfumo wote wa elimu nchini hivyo anatoa mwanya kwa watafiti wengine kujielekeza katika ngazi nyingine za utoaji elimu hasa elimu ya juu. Tatu, mbinu zaidi za kukusanya data zihuzishwe katika tafiti za usoni; matokeo yatakayotokana na mbinu hizo yanaweza kutumiwa kulinganisha matokeo ya utafiti huu uliotumia mbinu tatu. Nne, sampuli za wanafunzi kutoka viwango tofauti tofauti zitumike kwa nia ya kulinganisha hatua za kujifunza lugha zao lengwa. Hali kadhalika, tafiti za jinsi hii zifanywe kwa kutumia nadharia nyingine tofauti na nadharia ya hatua iliyofikiriwa kwa minajili ya kulinganisha matokeo haya na hata kubaini ikiwa matokeo ya jinsi hii yana umajumui wowote kwa kila anayejifunza lugha.

5.5 Hitimisho

Utafiti huu umefanikisha kupatikana kwa taarifa kuhusiana na mijadala inayohusu lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari hapa nchini Tanzania. Utafiti umetoa maoni ukishauri yafanyike mabadiliko ya lugha ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umeweka wazi sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari, umebainisha vikwazo vinavyoikikabili Kiswahili kisitumike kufundishia na kujifunzia masomo ya

sekondari. Pia utafiti huu, umetathmini mtazamo wa wanajamii kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari.

MAREJEO

Ajzen, I na Fishbein, M. (1980). *Understanding Attitudes and Predicting Social Behavior*. New York: Prentice-Hall Inc.

Akaka, L (2017). *Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya*. Kioo cha Lugha Juz.11 katika Journals.udsm.ac.tz

Babalola, E na Rotimi, T. (2009) *Code-Switching in Contemporary Nigerian Hip Hop Music*. Itupale Online Journal of African Studies.

Babbic, E. (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

BAKITA (1976). *BAKITA na Lugha ya Kufundishia*. Dar es Salaam: BAKITA.

Brock-Utne na wenzake (eds), (2003). *Language of Instruction in Tanzania and South Africa (LOITASA)*. Dar es Salaam: E & D Publishers.

Campbell, Z . M and Qorro, M (1987). *A Survey of the Reading Competence in English among Secondary School Students in Tanzania*. A Research Report funded by IDRC.

Campbell, Z. M na Qorro, M. A. S (1997). *Language Crisis in Tanzania*. The Myth of English Versus Education. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota

Chimerah, R. M (1998). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.

Chomsky, N (1986) *Knowledge of Language its nature and use*. Cambridge: Mass MIT Press.

Gorman, T. P. (1974). *The teaching of languages at secondary level: Some Significant Problems*. In W. H. Whitely (Ed.), *Language in Kenya* (pp. 481-545):. Nairobi: Oxford University Press.

Criper, C. and Dodd, W. (1984) *Report on the Teaching of English Language and its use as a Medium of Instruction in Tanzania*. Dar es Salaam: The British Council.

Galabawa, Justinian C. and Lwaitama, A. F (2005). *A Quasi-Experimental Study: A Comparative Analysis of Kiswahili and English as Languages of Instruction at Secondary Level in Selected Tanzania Schools*. In Brock-Utne, Birgit, Zubeida Desai and Martha

Qorro (Eds.). *LOITASA Research in Progress*. Dar es Salaam: KAD Associates.

Gorman, T. P. (1974). *The teaching of languages at secondary level: Some Significant Problems*. In W. H. Whitely (Ed.), *Language in Kenya* (pp. 481-545): Nairobi: Oxford University Press.

Herbert, R. K (1992). *Language and Society in Africa: The Theory and Practice of Sociolinguistics*. Witwatersrand: University PressWits.

- Kamwaga, E. (2023) *Kiswahili au Kiingereza? Lugha ya Kufundishia Inavyopasua Kichwa Tanzania*. Mchambuzi Tanzania katika [www.bbc.com>swahili>articles](http://www.bbc.com/swahili/articles).
- Kandagor, M. (2014). *Nafasi ya Kiswahili katika ushirikiano wa Afrika Mashariki*. Katika N. Michira, P. I. Iribemwangi na M. Mbatiah (Wah.), *Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na majukumu ya asasi mbalimbali* (uk. 180-192). Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Kiango, J. G. (2002). *Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya Afrika Mashariki*. [http://www.qucosa.de/fileadmin/ data/qucosa/documents/10082/9_12_kiango.pdf](http://www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documents/10082/9_12_kiango.pdf)
- Kihore, Y. M. (1983). *Nafasi ya Kiswahili Barani Afrika*. Katika D.L.W. Masoko na J.S.Mdee. (wah.). *MULIKA*. Na. 15, uk. 32-39.
- Kombo, D & Tromp, A (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Pauline Publications Africa.
- Kothari, C.R (2019). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing LTD.
- Lunyana, N.M (2015). *Haja ya Lugha ya Kiswahili Kutumika Kufundishia Elimu ya Sekondari: Mifano Kutoka Wilaya ya Ilemela – Mwanza*. Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria.

Malekela. G (2004). *Secondary School Student's Views on Medium of Instrucion in Tanzania*. Paper Presented at the LOITASA workshop 26-28 January. ArushaTanzania.

Massamba. D. P. B (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mekacha.R.D. K (2011). *Isimu Jamii.Nadharia na Mukdadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.

Mlama, P. na Materru, M. (1978). *Haja ya Kutumia Kiswahili katika Kufundishia Elimu ya Juu »' Lugha Yetu 35*. Dar es Salaam: BAKITA.

Msanjila, Y. P. (2004). *Kiswahili Kitumike Kufundishia Sekondari na Elimu ya juu Tanzania*. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila Y. P. na Wenzake (2009) *Isimu Jamii*. TUKI. Dar es Salaam.

_____ (2011) *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam:TUKI.

Mulokozi, M. M (2005) *Baadhi ya Vipingamizi vya Kiutawala vya Kutumia Kiswahili Kufundishia Sekondari na Vyuo*. Kioo cha Lugha. Vol.3 No1 (2005). University of Dar es Salaam.

Mwananchi (2021) Makweta Alikuwa sehemu ya Mafanikio katika Elimu.
<http://www.mwananchi.co.tz>

Mwinsheikhe, H (2003). *Using Kiswahili as a Medium of Instruction in Science Teaching in Tanzania Secondary School*. In Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds) *Language of instruction in Tanzania and South Africa*: E&D Limited.

Ng'waje. M. H. K (2019). *Lulu za Isimu Jamii: Mtazamo wa Kisinkronia kwa Sekondari na Vyu*. Mwanza: Tridax Africa Company Limited.

Nkapa, N. (1997). *Educational Research for Modern School*. Forth Dimension Publishing Company Limited. Enugu.

Onyango, J. O (1990). *Mielekeo ya Wasomi Kuhusu Matumizi ya Kiswahili Nchini Kenya..* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Kenyata.

Poplack, S. (2001). *Code – Switching (Linguistics)*. In Smelser Niel and Baltes, Paul (eds) *International Encyclopedia of the social and Behavioral Science*. Elsevier Science Ltd 2062.

Qorro M.A.S (2003). *Unlocking Language Forts. The language of Instruction in Post Primary Education in Africa with Special Reference to Tanzania*, In Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds) *Language of instruction in Tanzania and South Africa*: E & D Limited.

Radio Vatican (2020) Moja ya Lugha Iliyoenea katika Mataifa ya Afrika ni Kiswahili. Katika Kilele cha Maadhimisho ya Lugha Mama, UNESCO ya 27/02/2020 katika <https://www.vaticannews>

- Richard, J. C and Rodger, T. S (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching*. New York: Cambridge University Press.
- Rubagumya, C. M. (1990). *Language in Tanzania*. In Casmir Rubagumya (ed). *Language in Education in Africa*. England: Multilingual Matters Limited
- Rubagumya, C.M (2003).*English Medium Primary School in Tanzania. A New Linguistic Market in Education?* In Birgit Brock-Utne, Zubeida Desai and Martha Qorro (eds) *Language of instruction in Tanzania and South Africa*: E & D Limited.
- Rubanza, Y. I. (2002). *Realistic Revolutionary strategies in Harmonisation and Standardisation of African Languages*. In, Kwes Kwaa prah (eds.) *Rehabilitating African Languages*.The centre for advanced studies of African society. Cape Town
- Saleh, F. H (2019). *Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni Katika Darasa Mseto la Wingilugha*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wazungumzaji wa Lugha Nyingine (M.Ed. TEKSOL). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Sedlack, R.G. & Stanley, J. (1992). *Social Research: Theory and Methods*. Bouston: Allyn and Bacon.
- Senkoro, F. (2004). *The Role of Language in Education and Poverty Alleviation: Tool for access and empowerment in* Justian Galabawa and Anders

Narman Education poverty and Inequality (eds. Dar es Salaam. KAD Associates.

Sewangi, S.S. (2004). *Nafasi ya Lugha katika Maendeleo ya Uchumi: Mfano wa Kiswahili Kiswahili katika Tanzania*. Katika Kihore. y.M na Chuwa A.R(wah). Kiswahili katika karne ya ishini na moja. Dar es Salaam: TUKI.

Simala, I. (2001). *Kiswahili Katika Sayansi na Teknolojia. Katika N.I Shitemi na wenzie (ed). Kiswahili. A tool for Development*. Eldoret: Moi University University Press.

Tikolo, O. (2012). *English Language In Competency Amongst Senior Secondary School Graduates in Nigeria A-801: Education Policy Analysis and Research Utilization in comparative perspective*, Harvard Graduate School of Education.

Vuzo, M.S. (2002). *Pedagogical Implications of Using English as a language of instruction in Secondary Schools in Tanzania*. Report, No.9. Education in Africa. Vol.11 also: Institute for Educational Research

Wangari, M (2019). *Ukumbi wa Lugha na Fasihi: Vikwazo Vinavyokabili Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia*. Taifa leo (Daily Nation). Nairobi.

Williman, N. (2011). *Research Methods; The Basic*. New York: Routledge Taylorand Francis Group.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1995). *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Dar es Salaam

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar es Salaam.

Yoradi, S.Y. (2013). *Lugha ya Kiswahili Katika Kufundishia na Kujifunzia Elimu Shule za Sekondari*. Tasnifu ya Kutunukiwa Shahada ya Uzamili (M. A. Kiswahili). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

KIAMBATANISHO I

A: DODOSO YA WALIMU NA WANAFUNZI

TAARIFA TANGULIZI

Jina la shule..... kataWilaya ...

Hadhi yako: Mwalimu () Mwanafunzi ()

Jinsi: Me () Ke ()

- a) Zifuatazo zinaweza kuwa sababu zinazoshawishi matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya Sekondari?.Umepewa kauli tatu za kukubaliana,weka alama ya (√) kuonyesha msimamo wako.

Na.	Sababu ya matumizi ya Kiswahili	Nakubaliana	Nakataa	Sina hakika
1.	Kiswahili ni Lugha bora			
2	Lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo			
3	Ni lugha mama kwa wengi			
4	Kiswahili kina msamiati toshelevu			
5	Kiswahili ni Lugha muhimu			
6	Kiswahili kinaeleweka kwa urahisi			

b). Vifuatavyo vinaweza kuwa vikwazo vya kuzuia matumizi ya Kiswahili kufundishia na kujifunzia masomo ya Sekondari? Umepewa kauli tano za kukubaliana, weka alama(√)kuonyesha msimamo wako.

Na.	Vikwazo vya Kiswahili kutotumika	Nakubaliana sana	Nakubaliana	Sina uhakika	Nakataa	Nakataa kabisa
		5	4	3	2	1
1	Kulegalega kwa sheria ya lugha Nchini Tanzania					
2	Udhaifu katika asasi na Vyombo vya kukuza na Kuendeleza lugha ya Kiswahili					
3	Kiswahili kutokuwa na hadhi					
4	Kulegalega kwa sera ya lugha					
5	Msukumo mdogo kutoka kwa viongozi wa kisiasa					

KIAMBATANISHO II
MWONGOZO WA MAHOJIANO

Walimu, Wanafunzi na Wazazi

Na.	Maswali	Majibu	
1.	Unatumia lugha ipi kati ya hizi katika mawasiliano yako ya mara kwa mara? e. Kisukuma f. Kiswahili g. Kiingereza h. Lugha nyingine	Lugha	Idadi ya uchaguzi/marudio
2.	Una maoni yapi kuhusu lugha ya Kiswahili kutumika kufundishia na kujifunzia masomo ya sekondari. Chagua kauli moja kati ya hizi? f) Lugha ya Kiswahili inafaa sana g) Lugha ya Kiswahili inafaa h) Lugha ya Kiswahili haifai sana i) Lugha Kiswahili haifai j) Sina uhakika	kauli	idadi ya uchaguzi/marudio
3.	Eleza kwa kifupi sababu za uchaguzi wako katika swali la 2?		

Appendix 11.16

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA
DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES
REQUISITION FORM FOR RESEARCH CLEARANCE LETTER

Date: 2.05.2022

1. Name of Student PHILEMON, Joseph
2. Gender M
3. Registration No. PG 201900238
4. Faculty SANAA NA SAYANSI YA JAMII
5. Programme MASH
6. Title of Research MTAZANO KUHUSU KUFUNDISHA NA KUJIFUNZA NASOMU YA SEKONDARI KWA LUGHA YA KISWAHILI UCHUNGUZI KUTOKA WLAYA YA KWIMBA MKOANI MWANZA
7. Tentative dates of data collection: From 9/5/2022 to 23/5/2022
8. Student Email Joseph.Philemon81@gmail.com
9. Student Phone Number 0753115888
10. Research Location / Site: WILAYA YA KWIMBA Mkoa wa Mwanza

S/N	Region	District Council Municipality	Name of Organization	Postal Address	Place
1.	MWANZA	KWIMBA	MWANDEU SEKONDARI	88-NGUNDU	MWANDEU
2.	MWANZA	KWIMBA	MALYA SEKONDARI	88-NGUNDU	MALYA
3.	MWANZA	KWIMBA	TALLO SEKONDARI	88-NGUNDU	TALLO
4.	MWANZA	KWIMBA	MALIGISU SEKONDARI	88-NGUNDU	MALIGISU
5.					
6.					

11. Date of submission
12. Comments by Supervisor Ready for Data Collection

Name of Supervisor Dr. Salma Hamad Signature *[Signature]* Date 05/05/2022

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

DIRECTORATE OF POSTGRADUATE STUDIES

P.O. Box 23409
Dar es Salaam, Tanzania
<http://www.out.ac.tz>



Tel: 255-22-2668992/2668445
ext.2101
Fax: 255-22-2668759
E-mail: dpgs@out.ac.tz

Our Ref: PG201900238

27th May 2022

District Executive Director (DED),

Kwimba District Council,

P.O Box 88,

~~DAR ES SALAAM.~~ **MWANZA**

RE: RESEARCH CLEARANCE

The Open University of Tanzania was established by an Act of Parliament No. 17 of 1992, which became operational on the 1st March 1993 by public notice No.55 in the official Gazette. The Act was however replaced by the Open University of Tanzania Charter of 2005, which became operational on 1st January 2007. In line with the Charter, the Open University of Tanzania mission is to generate and apply knowledge through research.

To facilitate and to simplify research process therefore, the act empowers the Vice Chancellor of the Open University of Tanzania to issue research clearance, on behalf of the Government of Tanzania and Tanzania Commission for Science and Technology, to both its staff and students who are doing research in Tanzania. With this brief background, the purpose of this letter is to introduce to you **Mr. JOSEPH, Philemon, Reg No: PG201900238** pursuing **Master of Arts in Kiswahili (MA Kisw)**. We here by grant this clearance to conduct a research titled **“Mtazamo Kuhusu Kufundisha na Kujifunza masomo ya Sekondari kwa Lugha ya Kiswahili; Uchunguzi Kutoka Wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza”** He will collect his data at your area from 30th May 2022 to 15th July 2022.

In case you need any further information, kindly do not hesitate to contact the Deputy Vice Chancellor (Academic) of the Open University of Tanzania, P.O Box 23409, Dar es Salaam. Tel: 022-2-2668820. We lastly thank you in advance for your assumed cooperation and facilitation of this research academic activity.

Yours,

THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

Prof. Magreth S. Bushesha
DIRECTOR OF POSTGRADUATE STUDIES.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na. MZA/KDC/T.10/13 VOL.II/264

30 Mei, 2022

Bw. Joseph Philemon,
Mratibu Elimu Kata,
Kata ya Mwandu.

YAH: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI

Tafadhali rejea somo la barua hii,

2. Napenda kukujulisha kwamba, umeruhusiwa kufanya utafiti kuhusu **"Mtazamo kuhusu kufundisha na kujifunza masomo ya sekondari kwa Lugha ya Kiswahili; Uchunguzi kutoka Wilaya ya Kwimba"** katika Shule za Sekondari Malya, Mwandu, Tallo na Maligisu kuanzia tarehe 30/05/2022 hadi 15/07/2022.
3. Aidha, unashauriwa kuzingatia, Sheria, Kanuni, Miongozo na miiko wakati unafanya utafiti wako.

Nakutakia kazi njema.

Samwel Kulinga

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

K.N.Y. MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA
KWIMBA

Nakala Wakuu wa Shule za Sekondari,
Malya, Mwandu, Tallo na Maligisu - Mpatieni ushirikiano.